# MIFICHAMO KATIKA MASHAIRI YA MRISHO MPOTO:

## *NIKIPATA NAULI*

## NA

## *SIZONJE*

NYAMBOGA, DANIEL

TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI.

2018

A1804360A
2018 theses

# UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada ya uzamili katika chuo kingine chochote.

______________________ 23/11/2018

DANIEL NYAMBOGA Tarehe

( Mtahiniwa)

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa kazi hii walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.

______________________ 26/11/2018

PROF. JOHN H. HABWE Tarehe

( Mtahini)

______________________ 23.11.2018

PROF. K.W. WAMITILA Tarehe

(Mtahini)

**TABARUKU**

Enyi watu wa jana, baba na mama, Nyamboga na Mosaisi

Enyi watu wa leo, ndugu wa toka nitoke, Joel, Martha na Isaiah

Enyi watu wa kesho, waja wa moyo wangu, Makena na wanetu.

**SHUKRANI**

Nampa heshima na shukrani Mwenyezi Mungu kwa kibali cha siha katika safari ya utafiti huu. Nawashukuru wazazi wangu Nyamboga Joseph na Mosaisi Josephine kwa malezi ya tangu na msaada wao wa kila namna hadi sasa.

Ningependa kuwashukuru wasimamizi wangu Prof. John H. Habwe na Prof. K.W Wamitila kwa maelekezo ya karibu ya kila siku hadi kukamilika kwa tasnifu hii. Nawashukuru wahadhiri wangu,Dkt.Amiri Swaleh, Dkt. Mbuthia Evans, Dkt. Jerono Prisca, Dkt. Jefwa Mweri, Dkt. Mwangangi wa Musyoka, Prof. Rayya Timmamy, Dkt. Ayub Mukhwana, Dkt. Zaja Omboga, Prof. Iribe Mwangi, Mwalimu Sanja Leo,Mwalimu Mary Ndung'u na Dkt. Bitugi Matundura kwa kuchochea ari ya usomi katika lugha ya Kiswahili tangu shahada ya kwanza. Shukurani pia kwa Dkt. Mungania, Prof. Kithaka wa Mberia, Prof. Mwenda Mbatiah, Dkt. Tom Olali, Prof. Abdulaziz Hassan, Dkt. Hannah Mwaliwa, Dkt. Lutz Diegner, Prof. Markus Egg , Bw.Henry Indindi, Bw. Samson Ongarora na wengineo kwa kuendeleza ari usomi maishani.

Wanafunzi wenzangu Janet Muthoni,Willy Lusige, Anusu, Sirengo, Njane, nyinyi ni watu wa nguvu! Namshukuru sana kwa dhati Philes Rioba kwa dhati ya moyo wa ukarimu wa kila siku. Nawashukuru pia wapenzi wa lugha ya Kiswahili katika shule ya wasichana ya Alliance, Binti. Nkonge, Bw. Borwo, Bw. Kuto, Bw. Glen, Bi. Muli,Bi.Menjo, Bi. Kilinda, Binti. Muthamia, Binti. Kaviti, kwa mapenzi na muumano wa mawazo katika kuchangizana katika lugha.

Wazalendo wote hawa wa lugha wamekuwa wa manufaa sana katika shughuli za kuhakikisha kuwa dau na ari yangu ya lugha ya Kiswahili imekuzwa na kurutubishwa. Mungu awabariki sana!

**ORODHA YA MICHORO**

Kielelezo cha usimbaji na mfichamo .......................................... Uk. 36

Kielelezo cha mchakato wa ufasiri wa kauli ................................ Uk. 38

## IKSIRI

Utafiti huu ulipania kuchunguza mifichamo katika mashiri mawili teule ya Mrisho Mpoto ya *Nikipata Nauli* na *Sizonje*. Kwa kutumia maoni ya Grice (1975) kuhusu kanuni za utaratibu wa ushirikiano wa kimazungumzo tuliaangalia jinsi ukiukaji wa kanuni za ukweli, idadi, uhusiano na namna unavyozua mifichamo katika kauli. Tulichunguza mashairi hayo teule ili kutambua kauli zinazokiuka kanuni za utaratibu wa ushirikiano wa kimazungumzo na kuhakiki mifichamo inayojitokeza kwa msikilizaji kutokana na ukiukaji wa kanuni hizo. Aidha tulionyesha namna mfichamo huo unavyochangia katika kukuza maudhui mbali mbali katika mashairi haya mawili. Utafiti huu, unapendekeza kutumia mtazamo wa kipramatiki-mitindo, wa kuhakiki kazi za kisanaa katika kuonyesha namna mtindo wa matumizi ya lugha wa Mrisho Mpoto ulivyochangia katika kuleta ukiukaji wa kanuni katika kauli zake. Aidha tuliangalia mchango wa mkutadha katika ufasiri wa maana za kazi za kifasihi. Kwa kufanya hivyo tuliona namna kanuni au maarifa ya kipragmatiki yalivyotumika kueleza maana katika kazi ya kisanaa, hasa ushairi.

## YALIYOMO

UNGAMO .......... ii

TABARUKU .......... iii

SHUKRANI .......... iv

ORODHA YA MICHORO .......... v

IKSIRI .......... vi

YALIYOMO .......... vii

SURA YA KWANZA .......... 2

1.0 UTANGULIZI .......... 2

1.1 USULI WA MADA .......... 2

1.2 TATIZO LA UTAFITI .......... 4

1.3 MADHUMUNI YA UTAFITI .......... 5

1.4 MASWALI YA UTAFITI .......... 6

1.5 SABABU ZA KUCHAGUA MADA .......... 6

1.6 UPEO WA UTAFITI .......... 6

1.7 UMUHIMU WA UTAFITI .......... 7

1.8 UDURUSU WA YALIYOANDIKWA .......... 8

1.9.0 MISINGI YA NADHARIA .......... 11

1.9.1 Kanuni ya Ushirikiano .......... 12

1.9.2 Kanuni ya Idadi .......... 12

1.9.3 Kanuni ya Ukweli .......... 12

1.9.4 Kanuni ya Uhusiano .......... 13

1.9.5 Kanuni ya Namna .......... 13

1.10.0 MBINU ZA UTAFITI .......... 15

1.10.1 Ukusanyaji wa data .......... 15

1.10.2 Uchanganuzi wa data na uwasilishaji wake .......... 16

SURA YA PILI .......... 17

2.0 DHANA ZA KIMSINGI KATIKA UTAFITI HUU .......... 17

2.1 UTANGULIZI ........................................................................................17
2.2 DHANA YA PRAGMATIKI ..........................................................................17
2.3.0 DHANA YA MFICHAMO NA UTARATIBU WA USHIRIKIANO ....................19
2.3.1 Mfichamo wa viwango ...............................................................................19
2.3.2 Mfichamo wa kaida ....................................................................................20
2.3.3 Mfichamo wa kijumla..................................................................................20
2.3.4 Mfichamo maalum......................................................................................20
2.3.5Mfichamo wa mazungumzo .........................................................................21
2.4 SUALA LA MUKTADHA KATIKA PRAGMATIKI.............................................23
2.5 DHANA YA USIMBAJI MAANA ..................................................................25
2.6 UMUHIMU WA MFICHAMO KATIKA KUJENGA MAUDHUI ..........................25
2.7 MKUTANO WA PRAGMATIKI NA TAALUMA YA MITINDO ..........................29
2.8 HITIMISHO ...............................................................................................31
SURA YA TATU ..............................................................................................32
3.0 UHAKIKI WA MIFICHAMO KATIKA SHAIRI LA NIKIPATA NAULI.....................32
3.1 UTANGULIZI ..............................................................................................32
3.2 NIKIPATA NAULI.........................................................................................32
3.3 UPINGAJI WA KANUNI YA UKWELI ............................................................33
3.4 UPINGAJI WA KANUNI YA IDADI.................................................................38
3.5 UPINGAJI WA KANUNI YA NAMNA ..............................................................41
3.6 UPINGAJI WA KANUNI YA UHUSIANO .........................................................43
3.7 HITIMISHO ................................................................................................44
SURA YA NNE.................................................................................................45
4.0 UHAKIKI WA MIFICHAMO KATIKA SHAIRI LA SIZONJE ................................45
4.1 UTANGULIZI...............................................................................................45
4.2 SIZONJE ....................................................................................................45
4.3 UPINGAJI WA KANUNI YA UKWELI ............................................................46
4.4 UPINGAJI WA KANUNI YA IDADI.................................................................49
4.5 UPINGAJI WA KANUNI YA NAMNA..............................................................51
4.6 UPINGAJI WA KANUNI YA UHUSIANO .........................................................52

4.7 HITIMISHO ..... 53
SURA YA TANO ..... 54
5.0 MATOKEO YA UTAFITI, MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO ..... 54
5.1 UTANGULIZI ..... 54
5.2 MUHTASARI WA MATOKEO YA UTAFITI NA HITIMISHO ..... 54
5.3 MAPENDEKEZO ..... 56
KIAMBATISHO I: Nikipata Nauli – Mrisho Mpoto ..... 57
KIAMBATISHO II: Sizonje - Mrisho Mpoto ..... 61
MAREJELEO ..... 65

## SURA YA KWANZA

### 1.0 UTANGULIZI

Katika sura hii tutaanza kwa kutoa usuli wa utafiti huu, tatizo la utafiti, madhumuni ya utafiti, sababu ya kuchagua mada ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, upeo na mipaka ya utafiti,udurusu wa yalioandikwa kuhusu utafiti huu kisha tutaangalia mbinu za utafiti zitakazotumiwa kukusanya data, kuchanganua data na kisha kuwasilisha matokeo ya utafiti.

### 1.1 USULI WA MADA

Mnyampala (1964), anasema kwamba, "... mashairi ni baba na mama wa lugha zote zile zilizoko duniani, maana ni pambo au stara ya kila lugha..." zaidi ya haya, Mnyampala anaendeleza kwa kusema kuwa " ...utunzi wa mashairi ulianza zamani sana na hayachakai, yazidi kukua na kuzidi utamu na taalimu ya utungaji wake na kutukuzwa."

Mashairi yamekuwa nyenzo muhimu ya kupitisha ujumbe katika jamii tangu zamani, hasa kwa sababu, yanagusia masuala yanayoiathiri jamii katika maisha ya kila siku aghalabu pale mashairi yanapoghaniwa huwa na athari ya kudumu katika fikira za msikilizaji, ujumbe wa shairi hunata zaidi na maana zilizofumbwa katika shairi hujitokeza vyema zaidi.

Kwengineko, sifa muhimu za mawasiliano ya binadamu ni katika mazungumzo yao. Mazungumzo, kama tendo linalotokea kila mara katika maisha ya binadamu, husheheni kanuni fulani maalum za kidiskosi. Baadhi ya hizi kanuni zikiwa ni uteuzi wa mada, kukubaliana katika mazungumzo na welewa wa maana za kauli. Na ndivyo ilivyo pia katika ushairi na utungaji wa mashairi. Hata hivyo, ili kuelewana kimaana au kimaudhui, wazungumzaji lazima wafuate utaratibu fulani wa kiuelewano.

Grice (1975) anauita utaratibu huu utaratibu wa ushirikiano wa kimazungumzo na una kanuni nne muhimu. Kanuni ya idadi, ukweli, namna na ile ya uhusiano ambazo huelekeza namna wazungumzaji wanafaa kutekeleza mazungumzo yao kwa jumla. Kusema hivi ni kumaanisha kuwa, kanuni hizi za utaratibu wa ushirikiano zinaweka maagizo fulani kwa wazungumzaji ili wajikite tu katika kauli ambazo zinaendana na ushirikano katika mzungumzo. Isitoshe wazingatie muktadha ili kuweka wazi maana zinaziweza kutokea kutokana na kauli zao. Suala la muktadha

linatuingiza katika uwanja wa pragmatiki ambao Habwe na Karanja (2004) wanaeleza kuwa, ni maana ya kimatumizi au maana kimuktadha/mazingira.

Pana uhusiano mkubwa kati ya pragmatiki na fasihi kama anavyosisitiza Levinson(1983:376). Anasema kuwa, maarifa ya kipragmatiki yanaweza kutumika katika nyanja zote ambazo zinaangazia namna kauli zinavyoeleweka. Fasihi ni mojawapo ya nyanja hizo. Maoni haya ya Levinson, yanakubaliana na yale ya Scott (1977:126), ambaye anasema kwamba, sheria za mawasiliano au mazungumzo zinaweza kutumika katika mazungumzo yoyote bila kujali mada husika katika mazungumzo hayo au nyanja ya mazungumzo hayo. Kwa hivyo basi, kwa namna mazungumzo yalivyo katika kazi ya kisanaa, ujuzi wa kipragmatiki na dhana za kipragmatiki zinaweza kutumiwa kuhakiki mawasiliano na welewa wa kazi za kishairi ambazo ni kipera muhimu cha fasihi ya Kiswahili.

Kila tunaposema kauli au maneno yoyote katika usemi, huwa tunasema labda bila kuwa na fahamu maana zinazoweza kutokana na kauli hiyo. Au baadhi ya kauli nyingine tunajua maana tunavyozisema kwa malengo fulani mahususi katika akili zetu. Kwingineko, inatokea kuwa, msemaji anatoa kauli ambayo haijazingatia utaratibu wa ushirikiano ambao unafaa kuongoza msikilizaji kufasiri maana ya kauli ya msemaji. Kwa hivyo msemaji anasemekana kuwa amevunja au kukiuka kanuni za utaratibu wa ushirikiano wa kimazungumzo katika kauli yake. Pale ambapo, kanuni moja au zaidi inakiukwa katika kauli, basi mawasiliano yanachukua mkondo mwingine wa ufasiri wa maana iliyokusudiwa, labda kwa ukisio au kwa mfichamo. Kwa mfano;

(1) **Bora kujenga daraja kuliko ukuta**

kauli hii ina maana ya kisemantiki kwamba,

*Ni heri mtu kujenga kivukio mahali kuna mto au ufa kuliko kujenga kizuizi.*

Kwa upande mwingine, kauli hii imepinga kanuni ya utaratibu wa ushirikiano ya ukweli, kwa maana kuwa maneno *daraja* na *ukuta* yametumika kisitiari. Matumizi ya sitiari katika kauli hii yanafumba maana nyingine za kauli hii na hivyo maana nyinginezo zitakazoibuka ni maana za kimfichamo ambazo zitategemea ufasiri wa

msikilizaji pamoja na muktadha. Kama vile, baadhi ya maana zitakazotokana na kauli hii ni;

- *Usisahau ulikotoka kwa kukata mawasiliano*
- *Usiwapuuze waliokusaida awali kufikia upeo wa leo*
- *Ni bora kuwa na uhusiano mwema na watu kuliko kujitenga na watu*
- *Kimkutadha, sentensi hii ina maana kuwa viongozi wawe na wajenge uhusiano mwema na raia waliowachagua kuliko kujitenga nao.*

Ni uibukaji huu wa maana nyingi kutokana na ukiukaji wa kanuni za utaratibu wa ushirikiano, ambapo tunasema kuwa, msanii ametumia mtindo huu katika kuzua maana nyingi katika mashairi ya *Sizonje* na *Nikipata Nauli,* ili kusisitiza maudhui kadha katika nyimbo hizi. Hii ndio nia kuu ya utafiti huu, ile ya kuchunguza maana zinazoibuka kutokana na upingaji wa kanuni za utaratibu wa ushirikano na namna mtindo huu unavyokuza maudhui ya nyimbo hizi.

Mrisho Mpoto ni msanii wa Tanzania ambaye alizaliwa Songea na kusomea shule ya Ilala- Boma. Mrisho Mpoto kama mshairi ametunga mashairi mengi. Tunaweza kuyaweka mashairi yake katika matapo mawili makuu, yaani, mashairi yenye sitiari ya safari na mashairi kumhusu mhusika mkuu Sizonje ila katika utafiti huu tutashughulikia mashairi teule mawili – *Nikipata Nauli* na *Sizonje*. Ni matarajio yetu kwamba utafiti huu, utaweza kuendeleza mjadala kuhusu mtagusano uliopo kati ya isimu, hasa pragmatiki na fasihi na kazi za kisanaa kwa jumla.

## 1.2 TATIZO LA UTAFITI

Ushairi wa Mrisho Mpoto umejitokeza kuwa na mtindo wa kipekee katika uwasilishaji wake katika hadhira. Utafiti huu ulidhamiria kuchunguza ushairi wa Mrisho Mpoto kwa kuwa mashairi yake yana sifa za ufumbaji na mazungumzo katika uwasilishaji wake.

Katika juhudi za kuchunguza maana zinazotokana na mafumbo katika mashairi ya Mrisho Mpoto, tuliangalia maana za kimfichamo zilizojitokeza kutokana na kauli za msanii katika mashairi haya. Tulitumia mtazamo wa kipragmatiki-mitindo uliotuwezesha kuyaweka mashairi haya ya *Nikikipata Nauli* na *Sizonje* katika muktadha wake ili kuchunguza maana mbali mbali za kimfichamo zinazotokana na kauli za msanii katika azma yake ya kujenga maudhui.

Ni matarajio yetu kwamba, mbali na jukumu la kuwaburudisha wanajamii, mshairi ya *Nikipata Nauli na Sizonje* yana maudhui mengi muhimu ambayo yamefumbwa katika kauli za msanii Mrisho katika mashairi haya. Ujumbe huu utapatikana iwapo tutayachunguza mashairi haya kwa kina ili kufumbua maana za kimfichamo zinazotokana na kauli hizo.

Kuchukulia maana za kauli zinazotolewa na Mrisho Mpoto katika mashairi yake kijuujuu hakutoshi kuchambua maana iliyokusudiwa. Aghalabu inatubidi tuelewe maana ya misimbo hii kwa hujikita katika miktadha mbali mbali ya kijamii – yaani ya Afrika Mashariki na kwa jumla jamii lugha ya Kiswahili.

Ni kutokana na hali hiyo basi, maarifa ya kipragmatiki na maarifa ya mitindo ya kifasihi yanakutana ili kutoa ufafanuzi wa maana za kauli zinazotolewa na msanii katika mashairi haya mawili. Utafiti huu basi ilikuwa na nia ya kuchunguza maana za kimfichamo zinazojitozeka katika kauli za Mrisho Mpoto katika mashairi haya mawili na jinsi alivyofaulu katika kutumia mbinu ya kufumba maana pamoja na muktadha katika ukiukaji wa kanuni za utaratibu wa ushirikiano wa kimazungumzo.

## 1.3 MADHUMUNI YA UTAFITI

Madhumuni yetu katika utafiti huu ni kama yafuatayo:

i. Kuchunguza namna maoni ya Grice (1975) kuhusu upingaji wa kanuni za utaratibu wa ushirikiano yanavyoweza kutumika kipragmatiki-mitindo katika kueleza mtindo wa ufumbaji maana katika mashairi ya *Nikipata Nauli na Sizonje*.

ii. Kuhakiki namna muktadha unavyochangia katika kuchochea ufumbuzi wa maana za kauli mbali mbali katika mashairi teule ya *Nikipata Nauli na Sizoje*.

iii. Kuhakiki mifichamo ya kauli zinazopinga kanuni za ushirikiano wa kimazungumzo katika mashairi teule na namna kauli hizo zinavyoibua maudhui mbali mbali yanayojitokeza katika mashiri ya *Nikipata Nauli na Sizonje*.

## 1.4 MASWALI YA UTAFITI

Katika utafiti huu tulidhamiria kuongozwa na maswali yafuatayo;

i. Je, kuna athari yoyote ya kupinga kanuni za utaratibu wa ushirikiano wa kimazungumzo katika kauli za mashairi ya *Nikipata Nauli* na *Sizonje*?
ii. Je, kuna mchango upi wa matumizi ya mbinu za lugha katika upingaji wa kanuni za utaratibu wa kimazungumzo?
iii. Je, ni maana zipi za kimaudhui zinazojitokeza kutokana na upingaji wa kanuni za utaratibu wa kimazungumzo katika mashairi ya *Nikipata Nauli* na *Sizonje*?
iv. Je, ni nini mchango wa muktadha katika kufumbua maana ya kauli zilizopinga kanuni utaratibu wa ushirikiano wa kimazungumzo katika mashiri ya *Nikipata Nauli* na *Sizonje*?

## 1.5 SABABU ZA KUCHAGUA MADA

Mada hii iliteuliwa kwa kuwa itampa mtafiti nafasi ya kutumia mtazamo wakipragmatiki na ule wa kifasihi katika kuhakiki sanaa ya ushairi. Isitoshe mashairi ya *Nikipata nauli na Sizonje* yaliteuliwa kwa sababu ya usimulizi wake mzuri wa mtindo wa bayana wa mazungumzo, ukolevu wa lugha fasaha, sitiari na ishara zenye lugha nzito yenye mafumbo ya kumfikirisha msikilizaji pamoja na uwepo wa upana wa kimaana wa aina yake katika kufafanua maana ya nyimbo hizi.

Mashairi haya yaliteuliwa kwa kuwa yanaonyesha upekee wa kutumia muktadha katika usimulizi wake katika kufumba ujumbe aidha msanii ni mshairi aliye mstari wa mbele katika kukuza maenezi na usomi na utafiti wa lugha ya Kiswahili na fasihi yake.

## 1.6 UPEO WA UTAFITI

Utafiti huu utajikita katika mipaka ifuatayo;

Mrisho ameimba nyimbo za mafumbo zaidi ya kumi na mbili katika albamu tofauti tofauti. Tutachunguza usimbaji wa maana na mifichamo ya kauli katika nyimbo mbili pekee- *Nikipata Nauli* na *Sizonje*. Nyimbo hizi mbili zimeteuliwa kuwakilisha makundi makuu mawili ya sanaa ya

Mrisho Mpoto kufikia sasa, yaani, sitiari ya safari (kundi la kwanza) na mhusika Sizonje (kundi la pili).

Utafiti huu utajihusisha tu katika kauli za kimaandishi za mashairi ya Mrisho Mpoto na wala hautaangazia sifa kisimulizi, maigizo ya jukwaani ya nyimbo hizi, viziada lugha au mipando na mishuko ya toni ya mzungumzaji ambazo ni sifa zinazoweza kuchunguzwa kwa namna nyingine.

Utafiti huu utatumia maarifa ya fasihi na kipragmatiki katika kuchanganua nyimbo mbili za Mrisho Mpoto, yaani, *Nikipata Nauli* na *Sizonje.* Mfichamo utakaoshughulikiwa katika utafiti huu ni ule unaotokana na mtindo wa kufumba maana katika ujumbe au kuwasilisha kauli zilizofumbwa kwa kutumia mbinu mbali mbali za lugha.

Zipo nadharia mbali mbali za kifasihi ambazo zinaweza kutumiwa katika kuchanganua mashairi ya Mrisho Mpoto kimtindo na kimaudhui. Hata hivyo, utafiti huu utatumia mtazamo wa kati ya isimu na fasihi, ili kukisia maana za kimfichamo za mashairi msanii huyu, pamoja na kuangazia namna alivyofaulu kutumia mtindo wa ufumbaji maana.

Hatushughulikia kwa mapana mawanda mbali mbali ya semantiki na pragmatiki. Tutajikita tu katika maoni ya Grice (1975) ya nadharia ya mfichamo pamoja na kanuni za utaratibu wa ushirikiano wa kimazungumzo kama msingi wa kufanya uhakiki wetu.

## 1.7 UMUHIMU WA UTAFITI

Matokeo ya utafiti huu yatakuwa na umuhimu ufuatao;

Kwa kufafanua uhusiano kati ya upingaji kanuni za utaratibu wa ushirikiano wa kimazungumzo na uzuaji wa mifichamo ya kimazungumzo,tunatarajia kuwa utafiti huu utaweka wazi azma ya msanii ya kukiuka kanuni mbali mbali za utaratibu wa ushirikiano wa kimazumngumzo katika kauli zake katika mashairi yaliyoteuliwa.

Utafiti huu pia ni muhimu kwa kuwa utaendeleza msingi wa kuchanganua mashairi ya Kiswahili na kazi nyingine za kisanaa za Kiswahili katika mitazamo mbali mbali kando na ile ya kifasihi tu.

Utafiti huu pia utachangia katika kuonyesha muumano uliopo kati ya fasihi na isimu kwa kuwa sanaa ya Mrisho Mpoto itachunguzwa kipragmatiki.

## 1.8 UDURUSU WA YALIYOANDIKWA

Udurusu wa yaliyoandikwa utakuwa wa vitengo viwili: udurusu wa yaliyoandikwa kuhusu mfichamo /mifichamo ya mazungumzo na maoni ya wataalamu kuhusu mtazamo wa kipragmatiki-mitindo katika kuhakiki kazi za kifasihi.

Grice(1975) anadai kuwa, watu wanaposhiriki katika mazungumzo huhitaji ushirikiano kati yao ili mawasiliano yaweze kufanikishwa. Ushirikiano huu anaousema Grice una kanuni nne muhimu ambazo ni ukweli, idadi, uhusiano na namna. Kanuni hizi ndizo zinazoelekeza mazungumzo ya watu na pale kanuni hizi zinapokiukwa, maana za mifichamo hutokea.

Levinson (1983) anatoa mwanga zaidi kuhusu maoni ya Grice hasa kuhusu utaratibu wa ushirikiano katika mazungumzo na mifichamo ya mazungumzo pamoja na uwezo wa maelezo ya kipragmatiki katika miktadha ya matumizi ya lugha. Anasema kuwa "...kuna uwezekano kumaanisha zaidi ya yale yaliyosemwa..." Kwa maoni yake anadai kuwa "...tofauti kati ya mantiki na lugha asilia hupotea pale tu mfichamo wa kipragmatiki unapotiliwa maanani katika uhakiki wa matini..." Maoni haya ni muhimu katika kutusaidia kuchunguza namna kauli za msanii katika utafiti wetu zinavyomaanisha zaidi ya yale yanayosemwa.

Davies (2000:1-26), katika makala yake kuhusu maoni ya Grice kuhusiana na utaratibu wa ushirikiano katika mazungumzo, anaona kuwa ni vema kusoma kazi za Grice katika mkutadha wa kifalsafa kuliko kuzisoma katika miktadha tofauti. Anasema kuwa, "swala la mantiki, kaida na muhimu kabisa urazini lilirudiwa ruduiwa katika maoni ya Grice kuhusu mifichamo ya mazungumzo." Lengo la Davies ilikuwa ni kutafuta mantiki ya mazungumzo ambayo ingeweza kuelezea pengo kati ya kusema na maana, kusema na kumaanisha pamoja na maana za kaida na maana zisizo za kaida. Alibainisha kuwa mantiki hiyo aliyokuwa akiitafuta ni uwepo wa urazini katika mazungumzo. Kazi hii ni moja katika zile zitakazotuwezesha kujaza mapengo ya maana ya kauli za msanii katika utafiti huu.

Mey(2001:46) anasema kuwa " ...kama tutauliza swali, jibu ambalo kwa kweli halina maana,lina uwezo pia wa kuwa jibu la swali hilo." Ili kujua maana ya kauli, lazima msikilizaji afasiri kilichosemwa. Na kwamba, tatizo la fasiri hiyo ni kuwa ufasiri una uwezekano mkubwa wa kuibua maana zaidi ya moja kutokana na kauli. Anavyosema Leech(1981:30-31), "...kufasiri kauli ni

swala la kubahatisha kabisa au uundaji wa haipothesia." Ni maoni ya Leech kuwa, njia mojawapo ya kudumisha utaratibu wa ushirikiano katika mazungumzo, ni kwamba, inahitajika msemaji atoe taarifa nyingi ya kufahamisha iwezekanavyo ili kuepuka utata. Ufasiri wa kauli ili kupata maana mbali mbali ndio azma kuu katika utafiti huu, maoni ya kazi hii yana mchango mzuri.

Robyn (2004) katika tahakiki yake ya maandishi ya Levinson kuhusu maana za uchukulizi na mifichamo ya kawaida ya mazungumzo, anadai kwamba, hata kama Levinson anakubaliana na Grice kuhusu ukisiaji wa maana ambao unategemea sana muktadha katika mazingira ya kanuni za utaratibu wa ushirikiano katika mazungumzo, ili kupata maana iliyokusudiwa, anachukua msimamo tofauti, kwamba, pragmatiki ya maana ya kauli ni swala la uchukulizi ambalo linabebwa na fasiri za miundo ya kauli katika muundo wa lugha na si katika kigezo cha miktadha mahususi tu ya kauli hizo. Na hivyo fasiri za kauli hazijikiti katika uchanganuzi wa moja kwa moja wa kusudi la msemaji wa kauli bali katika matarajio ya jumla na namna lugha inavyotumiwa kikawaida. Maoni haya yanaongeza swala la miundo ya kauli katika kufasiri maana mbali na muktadha.

Kama inavyoonekana ni kuwa, utaratibu wa ushirikiano ndio hasa kiini cha nadharia ya mfichamo, na maoni mengi yanazunguka katika utaratibu huu wa ushirikiano katika mazungumzo kama ulivyosemwa na Grice (1975).

Grundy (2008:97) anasema, "...mfichamo hutokea kwa kuwa msikilizaji anachukulia kwamba msemaji anatilia maanani kanuni za utaratibu wa ushirikiano katika mazungumzo; hivyo, taarifa anayoitoa inataarifu iwezekanavyo, imeundwa vizuri, ina uhusiano kabisa na muktadha na inasemwa kwa namna nzuri ya kueleweka." Grundy hata hivyo anasema kuwa "...mbali na hayo ni kwamba, inawezekana kuwa msikilizaji anajua kuwa wasemaji mara nyingi hawatilii maanani kanuni za utaratibu wa ushirikiano katika mazungumzo na hivyo kanuni hizo aghalabu huvunjwa." Kwa maoni yake basi, kila kauli ina maana mbili, yaani ile maana asilia na maana isiyo asili( ambayo ni mfichamo ) hata kama kauli hiyo inazingatia kanuni ya utaratibu wa ushirikiano au la.Vile vile anadai kuwa ukiukaji wa kanuni za utaratibu wa ushirikiano ni mbinu ya kipekee ya kumfanya msikilizaji kukisia maana na hivyo kutambua mfichamo katika kauli. Kwa kifupi, upingaji wa kanuni za utaratibu wa ushirikiano, humweka msikilizaji tayari kuwa na mfichamo katika kauli zozote zile. Maelezo haya yanaonyesha ukweli uliopo katika uchanganuzi wa kauli ambazo zina maana pana.

Ochichi (2013) alishughulikia mfichamo na usimbaji maana kimazungumzo katika Kiswahili na Ekegusii katika tasnifu yake ya uzamili. Anaongezea swala la utamaduni na uwezo wa kiakili kama miktadha muhimu katika kufikia maana ya kauli zinazotolewa na msemaji. Hapa anasisitiza mawazo ya Wilson na Sperber (2002) kuhusu nadharia ya uhusiano. Mathalan, anasema "...chukulizi za uwazi wa kauli za kitamathali zimeonyesha kuwa maana ya msemaji haiwezi kuafikiwa kutokana na maana za maneno yaliyotumiwa. Hivyo basi, inabidi msikilizaji atumie ufahamu wa utamaduni na uwezo wake wa kiakili ili kufikia ufaafu wa jumbe zilizosimbwa kwenye kauli zenye tamathali za usemi." Kwa maoni haya, swala la utamaduni na uwezo wa akili ni muktadha ambao humsaidia msikilizaji kufasiri maana ya kauli.

Ndonye (2017) katika tasnifu yake ya uzamili, alishughulikia usimbaji katika mashairi *ya Rangi ya Anga* ya Kithaka Wa Mberia. Anaona matumizi ya rangi katika mashairi ya Kithaka wa Mberia kuwa ishara ya kusimba maana ambayo ni kama mtindo anaoutumia mwandishi huyu. Anaangalia ishara hizi na maana zake namna zinavyotafsiriwa na wanajamii.

Yuan (2017) ambaye alishughulikia uhakiki wa ushairi ya Bishop, ya *North Haven* na *Insomnia*, anasema kuwa, "...mtazamo wa kipragmatiki-mitindo ni wa baina ya taaluma nyingi ambao unalenga kukutanisha ama kuleta muumano wa mawazo yaliyotofautiana ya kiisimu na taaluma ya fasihi hususan katika kutumia nadharia ya kiisimu katika kuhakiki lugha inavyotumika katika kazi ya kifasihi. Katika utafiti wetu tuunapania kutumia maoni ya Grice kuhusu utaratibu wa ushirikiano na namna upingaji wa kanuni za utaratibu huu wa ushirikiano unavyojenga mtondo wa usimbaji maana na kisha tutachunguza mfichamo katika kauli zilizopinga kanuni hizo. Kwa kuangalia hivyo tutaeleza namna upingaji huu wa kanuni za utaratibu wa ushirikiano unavyomwezesha msanii Mrisho Mpoto kufikia azma yake ya kutumia mtindo wa kufumba maana katika mashairi yake.

## 1.9.0 MISINGI YA NADHARIA

Nadharia itakayoongoza utafiti huu ni ile ya mfichamo iliyoasisiswa na Grice (1975). Mchango wa Grice katika falsafa na isimu hasa mfichamo kimsingi ulianza mwaka wa 1961 katika makala yake ya Nadharia sababishi ya mtazamo (*The Casual Theory of Perception)* na uliendelea kukuzwa zaidi katika Mantiki na Mazungumzo *(Logic and Conversation)* mwaka wa 1967.

Grice alishikilia kuwa binadamu ni kiumbe wa kijamii sana na lazima azungumze na binadamu mwingine katika jamii kila mara isipokuwa pale anapokuwa na mazungumzo nafsi. Zaidi anasema kuwa wazungumzaji wananuia kushirikiana katika mazungumzo kwa hali zote, kwamba mawasiliano yana kitu kimoja muhimu ambacho ni ushirikiano katika mazungumzo kati ya msemaji na msikilizaji.

Kwa mujibu wa Grice, ushirikiano huu wa kimazungumzo unakuwa muhimu kwa sababu msemaji anajua kuwa, kauli yoyote atakayoitoa ina uwezekano mkubwa wa kuingilia haki za kibinafsi, matakwa na uhuru wa msikilizaji wake. Hii ndio maana tunafaa kuunda kauli zetu kwa namna fulani ambayo ina utaratibu wa kiushirikiano katika mazungumzo.

Kwa hivyo, Grice alitoa maoni kuwa, katika mazungumzo, kunahitajika utaratibu wa ushirikiano kila mara msemaji anapotoa kauli. Anasema, "...toa mchango wako katika mazungumzo kama inavyohitajika kwa kiwango ambacho unatokea, kwa lengo/kusudi linalikubalika au mkondo wa mazungumzo unayohusishwa nayo."

Robyn (2004) Mhimili mkuu katika nadharia ya mfichamo ni utaratibu wa ushirikiano katika mazungumzo, utafiti huu utatumia maoni hayo kuhakiki namna kauli za Mrisho Mpoto zinavyokaidi kanuni za utaratibu huu, hivyo basi kumfanya msikilizaji kuunda maana za kimfichamo kutokana na kauli.

Utaratibu wa ushirikiano wa Grice unatoa msururu wa kanuni ambazo zinatarajiwa kufuatwa iwapo watu watashirikiana ipasavyo katika mazungumzo yao. Kimsingi kanuni hizi ni nne ambazo zinafaa kufuatwa ili kushirikiana katika mazungumzo kwa azma ya kuelewana.

### 1.9.1 Kanuni ya Ushirikiano

Kuhusu kanuni hii Grice anamwelezea atoaye kauli kuwa:

"Uufanye mchango wako wa kimazungumzo jinsi inavyohitajika, katika mahali unapotokea, kulingana na mwelekeo au sababu inayokubalika ya mazungumzo ambamo unashiriki."

Kwa kuchukulia kuwa kanuni hii hutumika kila mara katika mawasiliano, Grice alitofautisha vipengee vinne vya matumizi maalumu ya kanuni hii chini ya kanuni au vikanuni mahususi. Kanuni hizo ni: Idadi, Ukweli, Uhusiano na Namna. Katika mifano hii, tutaelezea jinsi kanuni hizi zinavyoweza kuvunjwa na Uvunjaji huu ndio unaomfanya msikilizaji kujenga maana za kimfichamo.

### 1.9.2 Kanuni ya Idadi

a) Uufanye mchango wako uwe na ujumbe unaohitajika (kwa ajili ya mawasiliano ya wakati huo)

b) Usiufanye mchango wako kuwa na maelezo yanayozidi yanayotakikana.

Levinson (1983) anadai kuwa kanuni hii ya idadi huzua mfichamo za wastani. Kwa mfano,

(2) Mtu A: Jana si leo.

Msemaji wa tamko hili anatoa ujumbe finyu mno kuhusu anachosema. Hivyo basi, amevunja kanuni ya idadi na inamlazimu msikilizaji kujenga maana ya mfichamo. Mathalan, msemaji anasema haijaweka wazi ni nini kilichotendeka jana ambacho leo hakijatendeka au kivingine. Uchache huu wa habari unampa msikilizaji kuzua maana kwamba labda, leo kuna matumaini zaidi ya hali kuliko ilivyokuwa jana au hakuna matumaini namna ilivyokuwa jana.

### 1.9.3 Kanuni ya Ukweli

Jaribu kuufanya mchango wako kuwa wa kweli iwezekanavyo.

**Vikanuni**

a) Usiseme kile unachoamini ni uwongo.

b) Usiseme kile ambacho huna ushahidi wake.

Kwa mfano,

(3) Mtu A: Watu wa kijiji hiki wana shibe sana.

Ikiwa msemaji atatoa tamko hili akizingatia kanuni ya ukweli katika muktadha ambapo kijiji anachokirejelea kinakumbwa na baa la njaa, basi atakuwa amevunja kanuni hii ya ukweli. Hii inamaanisha kuwa, hataafikia uhusiano na msikilizaji. Hii ni kwa sababu si kweli kuwa watu wa kijiji hiki wana shibe. Kuvunja kwa kanuni hii ndiko kutamfanya msikilizaji kujenga mifichamo ambayo zitamwezesha kuelewa ujumbe uliosimbwa katika tamko hili. Kwamba msemaji hakutaka kusema moja kwa moja kuhusu hali ya kudhoofisha ya watu katika kijiji husika au msemaji anajaribu kukejeli hali ya uhitaji iliyoko kijini pale.

### 1.9.4 Kanuni ya Uhusiano

Kanuni hii inamwelekeza msemaji kutoa mchango unaohusiana na yanayozungumziwa (muktadha).

Grice anataja kuwa kuvunjwa kwa kanuni hii ni jambo linalotokea kwa nadra labda kwa sababu ni vigumu kutunga majibu ambayo yanaeleweka bila kuzingatia mada ya mazungumzo.

Kwa mfano,

(4) Mtoto (Nyakundi): Mama, nipe hela niende kutazama soka.

Mama: Nyakundi, umefika wapi katika kufanya kazi uliyopewa na mwalimu wako?

Mama hapa anakiuka kanuni ya uhusiano ili amweleze Nyakundi kwa namna isiyo ya moja kwa moja kuwa hawezi kumpa hela na hivyo hawezi kwenda kutazama soka kabla ya kumaliza kazi aliyopewa na mwalimu wake.

### 1.9.5 Kanuni ya Namna

Kanuni hii inamhitaji mzungumzaji kutoa mchango wake kwa jinsi iliyo wazi na inayoeleweka.

**Vikanuni vyake**

a) Sema mambo waziwazi
b) Jiepushe na utata
c) Kauli ziwe na mpangilio mzuri unaokubalika,

Kwa mfano;

(5) A: Ogeto alishiba kisha akala chakula chote.

Kauli kama hili inaenda kinyume na kanuni hii. Kushiba hakuwezi kutangulia kula chakula . Mtu hula kwanza ndio kushiba kuje baadaye.

Marmaridou (2000) anasema kuwa, kwa kuzingatia kanuni hizi, wanaozungumza wanazungumza kwa njia fanifu na ya kiushirikiano. Wanazungumza kwa chukulizi kuwa wasikilizaji wao wataongea kwa ukweli, kiuhusiano na kinachozungumziwa, na wazi wanapotoa ujumbe wa kutosha. La muhimu ni kuwa hata wakati ambapo mazungumzo hayaendelei kulingana na kanuni hizi, msemewa/msikilizaji huchukulia kuwa kanuni hizi zimezingatiwa katika viwango vya ndani zaidi na anatumia uwezo wake wa kufikiri kuchakata namna ambavyo kanuni ya ushirikiano inavyohusika.

Grice anaeleza kuwa kanuni hizi zinaweza kuvunjwa au kukiukwa katika mawasiliano ya binadamu. Hata hivyo, anasisitiza sharti kuwepo na ushirikiano. Namna moja ya kuzivunja kanuni hizi nimatumizi ya tamathali za usemi katika kauli.

Hivyo basi katika utafiti huu, tutajizatiti kuangalia namna mshairi Mrisho Mpoto anavyovunja kanuni hizi za mazungumzo kimakusudi ili kutimiza lengo lake ya kusimba maana katika mashairi yake. Usimbaji wa maana katika kauli ndio huzua mfichamo. Tunayaangalia mashairi haya ya Mrisho Mpoto kwa kuwa, ni mashairi ambayo yamejaa uzungumzi mwingi ndani yake.

Grice anasema kuwa kanuni za utaratibu wa mawasiliano zinapovunjwa kuna kusudi fulani, au ni kusema kauli hiyo kwa upole au lengo kwa lengo binafsi. Zaidi anasema kuwa kanuni yoyote inapovunjwa, kunazuka implikecha. Anatoa aina tano za mifichamo, ile ya viwango, mazungumzo, maalum, kaida na ile ya jumla.

Kuhusu mtazamo wa kipragmatiki-mitindo, huu ni mtazamo unaotumia maarifa ya pragamatiki na maarifa ya taaluma mitindo ili kuchunguza namna lugha inavyotumika katika kazi za kifasihi. Isitoshe mtazamo huu umetumiwa kuchunguza fani na maudhui katika kazi za kifashihi mbali mbali.

Yuan Li (2017) anatumia mtazamo huu ili kuchunguza namna kanuni ya utaratibu wa ushirikiano unavyotumika katika mashairi ya Bishop kama mtindo wa kuibua maudhui na athari za kiujumi. Alihitimisha kuwa, kwa kutumia nadharia ya kiisimu kuchunguza kazi ya kisanaa ya ushairi ni mtazamo wa kiubunifu wa kuweka daraja kati ya isimu na fasihi.

## 1.10.0 MBINU ZA UTAFITI

Utafiti huu ni kuhusu, uhakiki wa mfichamo unaoibuka kutokana na ukiukaji wa kanuni za utaratibu wa ushirikiano katika mashairi ya Mrisho Mpoto, msanii ambaye ameibukia Tanzania.

### 1.10.1 Ukusanyaji wa data

Utafiti wetu utakuwa wa maktabani. Tutadurusu matini zitakazokuwa na manufaa kwetu kama vile vitabu, tasnifu na majarida mbali mbali yanayoshughulikia dhana ya pragmatiki na mitindo mbali mbali ya kueleza mfichamo wa kauli. Aidha tutapitia kazi mbali mbali zilizoandikwa kuhusiana na kanuni za utaratibu wa ushirikiano wa kimazungumzo pamoja na kazi zilizotumia mtazamo wa kipragmatiki- mitindo kuhakiki ushairi.

Mbali na kusoma na kusikiliza nyimbo za Mrisho Mpoto, tutarejelea kazi za watafiti wengine waliohakiki suala la mfichamo katika ushairi.

Sampuli tutakayoiteua ni sampuli lengwa, ambayo itatokana na mashairi ya *Nikipata Nauli* na *Sizonje* ya Mrisho Mpoto. Kwa mujibu wa Mugenda na Mugenda (1999:50), aina hii ya sampuli hutumika katika utafiti unaokusudiwa kupata habari za kina kuhusu jambo fulani bila kujumuisha.

Kwa mujibu wa maelezo haya, tutachagua mashiri mawili teule ya Mrisho Mpoto; *Nikipata Nauli* na *Sizonje* ili kutusaidia kupata data maalum ya kauli zinazokiuka kanuni za utaratibu wa ushirikiano wa kimazungumzo tutakazozihakiki katika utafiti huu.

Mashairi haya mawili yatateuliwa kimakusudi kutoka sehemu mbili kuu za uimbaji wa msanii Mrisho Mpoto. Shairi la *Nikipata Nauli* litakuwa kiwakilishi cha sehemu ya kwanza ya uimbaji wa Mrisho kuhusu dhana ya safari. Shairi ya pili, *Sizonje* litawakilisha sehemu ya pili kuhusu mhusika *Sizonje*. Mashairi haya mawili yameteuliwa kwa kuwa yana data ya kutosha ya kukidhi mahitaji ya uchanganuzi wetu. Isitoshe, mashairi haya yana uzungumzaji mwingi ambao unatupa kigezo muhimu cha kutumia nadharia ya kanuni za utaratibu wa ushirikiano kimazungumzo kuhakiki kazi hii.

### 1.10.2 Uchanganuzi wa data na uwasilishaji wake

. Data ambayo tutapata katika utafiti wetu itachanganuliwa kwa misingi ya nadharia ya mfichamo ya Grice, kwa mtazamo wa kipragmatiki- mitindo.Data hii itatusaidia kujibu maswali yetu ya utafiti na madhumuni ya utafiti wetu. Matokeo ya utafiti huu yatawasilishwa kwa ripoti ya utafiti ambayo itakuwa ndiyo tasnifu yetu

## SURA YA PILI

## 2.0 DHANA ZA KIMSINGI KATIKA UTAFITI HUU

### 2.1 UTANGULIZI

Sura hii itachunguza dhana ya pragmatiki na dhana ya muktadha kama unavyojitokeza katika kueleza maana kauli. Tutaangalia namna usimbaji maana unavyofanikisha upitishaji wa ujumbe na ufasiri wa ujumbe kwa msikilizaji. Suala lingine la muhimu ambalo tutaliangazia ni nadharia ya mfichamo na maoni ya Grice kuhusu utaratibu wa ushirikiano. Isitoshe, tutaangalia umuhimu wa dhana ya mfichamo katika kufafanua maana za kauli katika matini au mazungumzo. Kisha tutaona ukuruba uliopo kati ya elimu mitindo na dhana ya pragmatiki.

### 2.2 DHANA YA PRAGMATIKI

Ni taaluma ya isimu inayochunguza namna lugha inavyotumiwa na wasemaji wake katika mazingira halisi (TUKI 2004).

Leech na Short (1971:290) wanasema kuwa, uhakiki wa kipragmatiki wa lugha unaweza kueleweka kwa jumla kuwa, uchunguzi wa dhana ya maana ambayo inatokana na namna kauli zinavyotumika na namna zinavyohusiana na muktadha ambapo zinatolewa na wala sio kutokana na sifa ama miundo ya maneno. Suala la muktadha ni kigezo muhimu ambacho tutatumia katika utafiti huu katika kupata maana mbali mbali za mifichamo za kauli.

Levision (1983) na Leech (1983) wanakubaliana kuwa, pragmatiki ni taaluma inayochunguza maana kimuktadha.

Aidha Levinson anadai kwamba pragmatiki ni taaluma inayohusu uhusiano uliopo kati ya lugha na muktadha, uhusiano ambao umefungamanisha sarufi ama misimbo katika muundo wa lugha husika. Maoni haya ni muhimu katika utafiti huu kwa kuwa yanatupa ufafanuzi wa namna ya kuchunguza kauli teule kipragmatiki.

Wales (1989:365), anaeleza "pragmatiki ni uchunguzi wa matumizi ya lugha unaohusika na maana ya kauli zaidi kuliko sentensi ya kisarufi." Vilevile maoni mengine kuhusu pragmatiki yanatolewa na Yule (1996:1) ambaye anasema kuwa, pragmatiki inahusu uchunguzi wa maana kama

inavyowasilishwa na msemaji(mwandishi) na kufasiriwa na msikilizaji(msomaji). Kwa maoni haya ni kuwa, msikilizaji wa kauli katika utafiti wetu ana uhuru wa kuipa kauli maana yoyote ile kama anavyoifasiri.

Wisnieski (2007) anaona pragmatiki kama uchunguzi wa maana ya maneno, virai na sentensi nzima na kwamba pragmatiki inajihusisha na maana ambayo maneno hupitisha wakati yanatumiwa au ile maana kusudiwa ya msemaji katika muktadha mahususi. Maelezo haya yanaendana na utafiti huu kwa kuwa yanajihusisha zaidi na ujumbe unaotokana na kauli zinazotolewa katika muktadha mahususi.

Maoni haya yanaelekea kuunga mkono madai kuwa, muktadha ni kigezo cha kimsingi sana katika kukisia maana ya kauli zinazotolewa na msemaji hasa pale maana za mfichamo zinapozuka. Kiukweli, pragmatiki haijihusishi tu katika maana ya maneno na sentensi (kama vile maana ya kisemantiki inavyofanya) bali inatilia maanani pia mahusiko ya muktadha kama kichangizi kikubwa katika kupanua upeo wa kuchunguza maana ya kauli. Kwa hivyo, muktadha una mchango katika kujenga mfichamo wa kauli mbali mbali katika mazungumzo na kwa jumla mfichamo huu hujenga maudhui katika kazi ya sanaa.

Hofmann(1993), anasema kuwa pragmatiki ni taaluma inayochunguza mapengo kati ya maana ya kawaida ya sentensi na wazo ambalo sentensi hiyo inapania kuwasilisha. Hofmann anadokeza kuwa mbinu za lugha kama vile chuku, sitiari,kejeli na kinaya zinapotumiwa katika kauli huvunja kanuni za utaratibu wa ushirikiano wa kimazungumzo. Aidha anadokeza kuwa kuzungumza kwa njia ya upole ni njia nyingine ya kuvunja kanuni hizo.

Kulingana na Hofmann, nadharia ya kanuni za utaratibu wa ushirikiano wa kimazungumzo una misingi yake kwa ukweli kuwa, mawasiliano ni jambo la kiushirikiano kati ya msemaji na mnenewa/msikilizaji. Kwa hivyo, msemaji lazima ateue maneno yake vizuri ili msikilizaji aweze kuelewe kusudi. Kwa upande mwingine, msikilizaji ana jukumu la kukisia kile anachokisema msemaji.

Ukiukaji wa kanuni za utaratibu wa ushirikani wa kimazungumzo huibuia mifichamo ya kimaana mbali mbali, kwa mfano;

## 2.3.0 DHANA YA MFICHAMO NA UTARATIBU WA USHIRIKIANO

Grice anadai kuwa, kanuni hizi za utaratibu wa ushirikiano, kama zivyokwisha kutajwa hapo awali, ndizo zinazozua pengo kati ya maana ya kisemantiki ya kauli na maana nyinginezo za kimfichamo zinazoibuka kutokana na kauli ya msemaji. Kimsingi, kanuni ya utaratibu wa ushirikiano inafaa kuelekeza namna diskosi asilia inapaswa kutendeka kulingana na Grice. Upingaji wa kanuni za utaratibu wa ushirikano pamoja na uzuaji wa mfichamo katika kauli ni mojawapo wa mchakato wa kuweka daraja katika pengo la kimaana lililoachwa na ujumbe uliosimbwa katika mazungumzo.

Kuhusiana na swala la mfichamo , Habwe na Karanja (2004) wanasema kuwa, ni dhana inayojitokeza pale mtu anasema kitu na kumaanisha kingine. Wanaongeza kwa kusema kuwa maana ya mfichamo hufasirika tu katika muktadha. Kwamba muktadha humfanya msikilizaji kuzua mfichamo wa kile ambacho kinasemwa na masemaji.

Isitoshe, kama anavyosema Levinson (1983), nadharia ya mfichamo inasaidia sana katika kuweka wazi ujumbe wa kisemantiki na ujumbe wa kipragmatiki katika maneno na sentensi. Ni katika uwekaji huu wazi wa maana ya semantiki na maana ya kipragmatiki ambapo maudhui mbali mbali yanajitokeza katika mashairi ya *Sizonje* na *Nikipata Nauli.*

### 2.3.1 Mfichamo wa viwango

Huu ni mfichamo unaotokana na idadi ya ujumbe ambao msemaji kauli anautoa.

Kwa mfano:

(6) Msemaji katika sherehe ya mazishi,

Mtu A: Kumbe Yohana alikuwa na watu watatu tu!

*Maana ya kauli*: Watu wachache wamehudhuria mazishi ya Yohana.

*Mifichamo ya kauli*: Yohana kwa maisha yake hakuwa na umaarufu chanya katika jamii

Msemaji anatumia kauli hii kama dhihaka ya kuwachokoza watu wa Yohana

### 2.3.2 Mfichamo wa kaida

Huu ni mfichamo unaotokea pale ambapo, msikilizaji tayari ana maana fulani ya matokeo ya kauli, labda kutokana na utamaduni au mazingira.

Kwa mfano:

(7) Mtu A: Peter amemwoa mwanamke mweupe.

*Maana ya kauli*: Peter amemwoa mwanamke wa rangi ya nyeupe

*Mfichamo wa kauli:* Peter amemwoa mwanamke mrembo au mzungu.

Kwamba katika mazingira haya, kikaida ni kuwa mwanamke yeyote mweupe ni mrembo na kwa hivyo wanawake wazungu wote ni warembo!

### 2.3.3 Mfichamo wa kijumla.

Huu ni mfichamo ambao hauhitaji muktadha katika welewa wake. Kwamba, msikilizaji hana haja ya kuweka kauli katika muktadha maalum ile kupata maana yake. Kwamba msikilizaji atakisia maana ya kauli kijumla tu.

Kwa mfano;

(8) Mtu A: Nilifika jana.

Msikilizaji wa kauli hii hana haja ya kuweka kauli hii katika muktadha wowote, maana iliyoko ni kuwa, msikilizaji aliwasili alipo jana.

### 2.3.4 Mfichamo maalum

Hii ni mfichamo ambapo msikilizaji anahitajika kuweka kauli katika muktadha maalum ili kuzua maana iliyoko. Kwamba, msikilizaji huwa ana muktadha wa awali, kama vile, habari za awali, ama ujuzi wa mazungumzo ya awali.

Kwa mfano;

(9) Mtu A: Umebeba?

*Mfichamo*: hili ni swali ambalo linaonyesha kuwa, msikilizaji huyu ana habari muhimu za mwanzo kuhusiana na kile ambacho angekibeba.

Vile vile katika muktadha wa lugha ya vijana wa nchini Kenya hasa wanawake, kauki hii italeta mfichamo kwamba msemaji anamuuliza mwezake iwapo ni mjamzito.

Aidha katika mazingira ya Kenya kwa wafanyikazi wa vibarua, kauli hii inaweza kuleta mfichamo wa kuiba bidhaa kutoka wanakofanyia kazi vibarua hawa wazungumzaji.

**2.3.5Mfichamo wa mazungumzo**

Marmaridou (2000) akimnukuu Grice (1975) anaeleza kuwa mfichamo wa mazungumzo ni fahamu ambazo huibuka wakati wa mazungumzo, kwa misingi ya *kanuni* fulani zilizo chini ya maingiliano ambazo wazungumzaji huonekana kuzingatia au kuvunja, huku *wakiwasiliana kiuhusiano* baina yao. Hivyo basi, mfichamo ni fahamu za kipragmatiki. Grice alianzisha imani kwamba, 'si kila ukweli kuhusu matumizi ya neno unaleta utambuzi wa moja kwa moja hadi kwenye maana ya neno'. Hata hivyo, utofauti wake thabiti kati ya kile kinachosemwa (semantiki) na kile kinachomaanishwa (uundaji wa implikecha) hauzingatii michakato ya kipragmatiki katika mawasiliano. Mfichamo ya mazungumzo hivyo basi, haihusishwi na usemi wowote ila kama kawaida hupata ufahamu kutokana na matumizi ya tamko fulani kutoka kwa muktadha (Levinson 1983)

Grice (1975) anasema ili kuwepo mantiki katika mawasiliano kuna michakato mbali mbali za kukubaliana kati ya watu wawili wanaoshiriki katika mazungumzo.

Kwa mfano;

(10) Mtu A: Jamani leo jua linawaka sana eh?

Mtu B: Kweli linawaka sana.

Hawa watu kwa kweli hawajuani. Ni kwamba wanajaribu kujenga uhusiano ili mazungumzo yao yawepo.

Levinson (1983) anataja kuwa nadharia ya Mfichamo ya Grice ni nadharia kuhusu namna watu wanavyotumia lugha. Anaendelea kueleza kuwa, mapendekezo ya Grice ni kuwa kuna seti ya

machukulio yanayoelekeza matendo katika mazungumzo. Grice anajitokeza na maelekezo manne ya kanuni za mawasiliano ambazo kwa pamoja hudhihirisha kanuni ya ushirikiano.

Kwa kijumla ni kwamba, kama alivyodai Robyn (2004), kwamba, kanuni za utaratibu wa ushirikiano ndio kiini hasa cha nadharia ya implikecha. Pale ambapo kanuni hizi zimekiukwa, basi huwa kumesimbwa maana, na hivyo msikilizaji huzuka na maana ya mfichamo wa kauli.

Ochichi (2013), akimtaja Thomas (1995), katika tasnifu yake ya uzamili anatoa ufafanuzi wa nadharia ya Grice inavyotumika kueleza mawasiliano kimazungumzo katika kiekelezo.

Wazo/nia ya msemaji + muktadha

↓

Msimbo

↓

Uzungumzaji

↓

Ufasiri wa kauli (Msikilizaji) + Muktadha

↓

Nia/wazo kueleweka na msikilizaji.

Mfichamo wa kauli za msemaji ni dhana katika taaluma ya pragmatiki inayoshughulikia maana inayoibuliwa baada ya mzungumzaji kupinga kanuni fulani za ushirikiano katika mazungumzo katika muktadha mahususi. Ukweli wa kauli hizi utategemea aina ya mfichamo ambao msikilizaji atajenga kutokana na kauli. Tutatumia kielelezo hiki cha kufasiri kauli katika kupata mfichamo katika maana zilizosimbwa katika mshairi ya Mrisho Mpoto.

Katika utafiti huu, tutaongeza katika kielelezo hiki, dhana ya upingaji wa kanuni za utaratibu wa ushirikiano kama kichocheo cha usimbaji maana kisha mifichamo inayotokana na misimbo mbalimbali ya kauli.

## 2.4 SUALA LA MUKTADHA KATIKA PRAGMATIKI

Kimsingi, muktadha ni mazingira halisi ya mazungumzo.Grice (1975), katika utaratibu wa ushirikiano, anatoa kanuni ya uhusiano ambayo inamhitaji mtoaji kauli ajikite katika muktadha wa mazungumzo ili aweze kuhusika kamili katika mazungumzo. Msikilizaji anapopata kauli yoyote, mwanzo anaiweka katika muktadha wake halisi ili kauli hiyo iweze kuleta maana.

Kulingana na Wilson na Sperber (2004), wanaona suala la muktadha kuwa ni kichochezi au kilipuzi kimojawapo kwa msikilizaji katika kufumbua maana ya iliyokusudiwa na msemaji. Kilipuzi hiki hutumika na msikilizaji kupima kauli ya mzungumzaji na kuifasiri vilivyo.

Mawazo wa Sperber na Wilson yanaelekea kuwa sawa na yale ya Akmajian (2001) ambaye anaeleza kuwa, ufasiri wa maana hufanyika katika akili za msikilizaji na hupitia mchakato ufuatao;

Wazo

↓

Uwezo wa utambuzi wa usemi

↓

Uwezo wa kuelewa mfumo wa kileksika na kisintaksia

↓

Uwezo wa ufasiri wa kisemantiki

↓

Uwezo wa kipragmatiki

↓

Utambuzi wa maana iliyodhamiriwa

Hivyo basi kauli inaposemwa, huwa inapita muktadha wa akilini ambapo fasiri za kisemantiki na kipragmatiki hutokea. Aidha fasiri za kipragmatiki mara nyingi hutokea kuwa zaidi ya moja kwa sababu ya maana zilizofichama au implikecha. Kwa namna hii maudhui hujengeka na msanii huwa amesema mambo mengi kwa kauli chache.

Habwe na Karanja (2004) wanasema kuwa maana ya muktadha wa kimatumizi hutilia maanani sana maana kisarufi.Neno huangaliwa kulingana na muktadha ambamo limetumiwa. Aidha wanasema kuwa, kile mtu anachokisema si lazima awe ndicho anakimaanisha. Kwamba kile anachokisema ndicho maana ya kimsingi ya kauli yake na kile anachokimaanisha ndicho maana ya muktadha.

Wamitila( 2008) anasema kuwa, "...muktadha wa tamko fulani unaathiri kwa kiasi kikubwa maana ya tamko lenyewe au jinsi litakavyofasiriwa na anayelisikiliza...". Aidha anadai kuwa muktadha huu unaweza kuwa muktadha asili au pokezi. Maana ya kazi ya fasihi lazima itilie maanani uhalisi wa jamii kama vile; mivutani ya kitabaka, kiuchumi, kihistoria au hata ile ya uzalishaji.

Muktadha ni kichocheo muhimu sana katika kuzua maana za mifichamo akilini mwa msikilizaji. Kwa mfano, hebu tuchukulie msemaji ambaye amemwona mpita njia akiwa amevaa koti chafu na anajaribu kutoa kauli kwa msikilizaji wake.

11) **Mtu yule ana koti safi sana.**

Katika muktadha huu ambao, msikilizaji anaona kwa kweli koti la mzungumziwa ni chafu, lakini msemaji amaamua kuliita safi, hana budi ila kupata maana nyingine inayoibuka ya kauli hii, zaidi ya kile alichokisema msemaji.

Kwamba msikilizaji ana namna nyingi ya kufasiri kauli hii lakini kutokana na muktadha wa kauli, msemaji huyu ametumia kejeli ili kukidhi mahitaji yake ya kutoa ujumbe huu kwa namna hiyo, ili msikilizaji ajijazie mwenyewe.

Kwa mfano msanii anaposema kauli ifuatayo katika *Nikipata Nauli* kuwa;

12) **Nasikia wageni wamefurahi sana kusikia sauti yako**

**Tena wanafurahishwa na ule ubeti wa mwisho uliouongeza**

**Wa mbio zetu kutoka uhuru mpaka hapa tulipo**

Kulingana na muktadha wa mataifa ya Afrika Mashariki, msikilizaji wa kauli hii, atazua maana zaidi ya moja kwa sababu kauli hii inazua mfichamo. Mathalan, *wageni hawafurahishwi na historia ndefu za maendeleo duni ya nchi au kiongozi huyu hana haja ya kurudia rudia historia ya nchi kwa wageni bali awaonyeshe maendeleo yaliyofikiwa.*

Mbali na muktadha, mbinu za lugha za kifasihi pia huwa vichocheo muhimu katika kuonyesha kauli inazua mfichamo. Mbinu kama sitiari, chuku, kejeli, tashtiti pamoja na maswali ya balagha ni vionyeshi vya uwepo wa maana ya ziada katika kauli. Mbinu hizi zinapogundulika katika kauli huwa na ishara tosha ya kumuashiria msikilizaji kupata maana nyingine zaidi ya mipaka ya yale yaliyosemwa.

Katika muktadha wa mashairi teule ya Mrisho, msanii ametumia lugha inayofumba maana kwa namna inayozua mifichamo mbali mbali ambayo inawachochea wasikilizaji wake kufikiria na kujifasiria maana kutokana na kauli zake.

## 2.5 DHANA YA USIMBAJI MAANA

Usimbaji maana ni mtindo wa kupitisha ujumbe kutoka kwa msemaji hadi kwa msikilizaji wake kama wanavyosema Sperber na Wilson (2004). Kwamba msemaji anatoa kauli yake katika msimbo wa maana kupitia nyenzo fulani mahususi ama kwa ishara au kwa maneno akiwa na kusudi la kupitisha ujumbe fulani. Mbali na kutoa tu msimbo wa kinachokusudiwa, msemaji pia hutoa ushahidi fulani wa kusudi la msimbo wake ili msikilizaji kufasiri ujumbe wa kauli hiyo kwa urahisi kutokana na ushahidi huo.

Grice anachukulia ushahidi huu kama matarajio ya msikilizaji ambayo kila mara kauli inaposemwa, msikilizaji anatarajia kuwa msemaji amezingatia matarajio hayo. Matarajio haya ndiyo Grice anayoyatoa katika kanuni ya utaratibu wa ushirikiano.

## 2.6 UMUHIMU WA MFICHAMO KATIKA KUJENGA MAUDHUI

Katika sehemu hii, tunajaribu kutoa maelezo namna kauli zinavyofumbwa kutokana na upingaji wa kanuni za utaratibu wa ushirikiano kisha kutoa mwanga kuhusu maana ya kisemantiki na fasiri nyingine za kimfichamo zinazozuka kutokana na muktadha wa mashairi teule ya Mrisho.

Kimsingi, kauli inapotolewa huwa ina maana yake ya kisemantiki lakini usikilizaji na ufasiri wa maana ya kauli hiyo hutegemea mambo mengi mojawapo ikiwa muktadha/mazingira. Ile maana inayozuka kutokana na msikilizaji baada ya kauli kupitia michakato ya uelewaji na ufasiri inazua suala la mfichamo. Hivyo basi dhana hii ya mfichamo haina umuhimu tu katika kuweka daraja ya maana ya mzungumzaji na ile ya msikilizaji bali pia katika kurahisisha mawasiliano kati ya watu wawili au kati ya msemaji na hadhira yake kwa kuhalalisha kuwepo na maana nyingine za ziada za kauli.

Dhana ya mfichamo inatokea kuwa mfano mzuri wa hali na uwezo mkubwa wa taaluma ya pragmatiki kueleza mambo ya isimu kwa jumla na yale ambayo yapo nje ya isimu na mpangilio ya kikaida wa lugha. Kama vile upingaji wa kanuni za utaratibu wa ushirikiano, mtagusano wa

mzungumzaji na msikilizaji katika mawasiliano pamoja na athari zake katika lugha kwa jumla. Kwa hivyo basi suala la mfichamo hutoa maelezo muhimu ya kimatumizi kuhusu dhana za kiisimu. Kwa mfano;

(13) **Msemaji A:** ***Sizonje, hii ndio nyumba yetu…***

Kauli hii namna ilivyo ni kwamba, msemaji anamwambia msikilizaji wake (Sizonje) kwa haja ya kumwonyesha nyumba yao kwa kuashira, na hii ndio maana yakikaida kauli hii.

Hata hivyo kwa kuzingatia dhana ya mfichamo, kauli hii imepinga kanuni za utaratibu wa ushirikiano kwa kutumia sitiari. Kanuni ya ukweli imepingwa, kwa maana kuwa, kiukweli, kile anachoambiwa akione Sizonje, si lazima kiwe ni nyumba halisi. Maoni haya yanaonekana tu pale pragmatiki au suala la maana kimuktadha linapotiliwa maanani. Mathalan,

(i) *Maana ya msemaji;*- ***Hii ndio nyumba yetu (yaani mjengo fulani wanamokaa watu).***

*Maana ya msikilizaji (mifichamo);* - Hii ***ndio serikali yetu***

- ***Hii ndio ikulu yetu***
- ***Huu ndio uongozi wetu tunaokurithisha***
- ***Hii ndiyo ndoa yetu n.k***

Mifichamo hii ni kichangizi muhimu katika kutubainishia ujumbe zaidi wa kauli na hivyo kuufanya kueleweka zaidi. Kwa kufanya hivi, dhana ya mfichamo inaeleza namna kauli zinaweza kuwa na maana zaidi ya moja kwa kuzingatia muktadha husika na upingaji wa kanuni za utaratibu wa ushirikiano.

Kwa maana hii, mfichamo huweka daraja katika nafasi iliyoachwa kati ya mambo mengi yalioachwa nje katika kauli ambayo hayakusemwa kwa kutoa upeo mkubwa wa maana kama ilivyo hapo juu.

Mfichamo vile vile ni muhimu katika kueleza upanuzi wa maana ya maneno mbali mbali katika mazingira tofauti. Hivyo basi iwapo maana ya maneno katika kauli inafaa kuelezwa kikamilifu, basi kuna umuhimu wa kuwepo kwa mfichamo . Kwa mfano, hebu tuliangalie maneno *"pole na hongera"* katika kauli hii inayotolewa katika shairi *Nikipata Nauli.*

(14) **Pole sana mjomba, una kibarua kizito kutaka dunia kuwa kijiji, Hongera!**

Neno *"pole"* katika hali ya kawaida ni kihisishi, cha kuonyesha huruma. Hii ni maana ya kisemantiki ya neno hili.

Katika kauli (14) hapo juu, neno (pole) limepinga maana yake ya kawaida, na kutokana na upingaji wa maana hii, kunatokea mfichamo wa maana zaidi ya moja ya kumaanisha. Mathalani katika muktadha wa shairi la *Nikipata Nauli*;

*"Pole"* - ni tamko la kikejeli kwa kiongozi ambaye amesahau majukumu yake katika jamii

-kumkumbusha kiongozi kuhusu ahadi alizozitoa akigombea wadhifa

-kumpa ujumbe kiongozi aliyechaguliwa, kuwa raia waliomchagua bado wanamhitaji ila hafikiliki.

Kwa upande mwingine neno *"hongera"* ni kihisishi vile vile ambacho hutoa maana ya kupongeza mtu kwa mazuri au kwa mafanikio fulani aliyoyafikia maishani. Ila katika muktadha wa shairi hili;

(15) ***"Hongera"*** – ni tamko linalototolewa kikejeli kumpongeza kiongozi kwa kufikia madarakani na kumsahau raia aliyemchagua.

Kwa kijumla ni kuwa, kanuni zinazozua mifichamo huchangia sana katika kutoa kwa upana kabisa maelezo ya mambo na dhana zisizouhusiana za kiisimu na fasihi. Kama vile namna jazanda, kejeli, isitiaris na mbinu nyingine za kisanaa zinavyotumika katika kazi ya sanaa.

Kutokana na maelezo haya, Portiner (2005) anadai kuwa, si kila mara msemaji kauli anamaanisha kile anachokisema, ndipo inapombidi msikilizaji wake kujijengea maana nyingine kwa kuwa ushirikiano wake wa kimazungumzo na msemaji ujumbe umepingwa. Pale kwa mfano, msemaji kauli anapoamua kutumia kinaya au sitiari katika kauli zake kimakusudi, huwa anapinga ushirikiano wake wa kimazungumzo na msikilizaji wake. Hili linampa msikilizaji wake haja ya kujenga maana mbali mbali kutokana na kauli. Kwa hivyo, tunaishia katika upanuzi wa maudhui au ujumbe unaosemwa katika mazungumzo.

Kama vile katika shairi la *Sizonje* msanii anatoa kauli kwa kusema;

(16) **Milango ipo, wanapita madirishani**

Tuzingatie hatua zifuatazo katika kuelewa kauli hii,

i. Tukichukulia msemaji kuwa (S) na msikilizaji kuwa ( L)

ii. Basi, S anatoa kauli ***Milango ipo, wanapita madirishani*** kwa L

iii. Na kwamba L anajua kuwa S yupo katika hali zake razini na hasemi kauli zake katika maigizo ya kuburudisha tu au kwamba S hasemi kutokana na athari za dawa za kulevya

iv. Na kwamba S anajua kuwa L anaelewa anachokisema kwa kuwa L anaweza kuzungumza na kuelewa kwa lugha ya Kiswahili maana kauli ipo kwa lugha ya Kiswahili

v. Hivyo basi S anajua kuwa L anajua haya yote, na hivyo anatoa kauli yake kwa haja ya kumaanisha kitu fulani au kutoa ujumbe fulani

vi. Kwa misingi ya utaratibu wa ishirikiano, L anaamini kuwa S anatoa kauli yake kwa msingi ya kiuelewano, yaani, anashirikiana naye kwa kuzingatia kanuni za ukweli, idadi, uhusiano na namna

vii. Mahitaji ya kimsingi ya kanuni ya ukweli, na kwamba kauli ya msemaji ijaribu iwezekanavyo kuzingatia ukweli

*viii.* Kwa hivyo, maana ya kisemantiki ya kauli ya S ni kwamba *watu wanapita madirishani hali milango ipo.*

ix. Kama hakuna sababu ya kufikiri kuwa S amepinga kanuni yoyote, basi L atatosheka na maana hii ya kisemantiki

x. Suala lingine katika ushirikiano kimazungumzo ni kanuni ya idadi

xi. Iwapo L atatosheka na habari alizozitoa S kuwa ndio habari muhimu zilizotakiwa, basi atatosheka na maana hiyo aliyoielewa

xii. Isitoshe, iwapo L atakubaliana na S kuwa, ndio,ni kweli watu hupita madirishani hali kuna milango katika mazingira hayo, basi kauli hii ina uhusiano na muktadha na kwamba imesemwa kwa namna nzuri na wala haina utata wowote

xiii. Lakini iwapo kauli hii itapinga ukweli uliopo wa kimuktadha, basi L atalazimika kujenga maana nyingine za kimfichamo , kama vile;

- kuna utaratibu wa kufanya mambo lakini watu wanapenda kutumia njia za mkato
- kuna njia nzuri ya kufikia huduma za serikali ila watu wanapenda rushwa
- watu wana tamaa ya kufikia ufanisi haraka katika nchi husika
- katika nchi hii kuna watu wanaotumia fujo ya kulazimisha mambo yatendeke wanavyotaka wao n.k.

Kutokana na mfano huu, Portiner anaona kuwa, nadharia ya Grice ya mfichamo na hasa kanuni ya utaratibu wa ushirikiano ni kielelezo cha kimawasiliano kinachopanua maana katika kauli na

kujenga maudhui zaidi pamoja na uelewekaji wa ujumbe katika kauli. Kwa ukweli huu basi maudhui katika mashairi teule ya Mrisho yanaeleweka zaidi kwa maana za kimfichamo zinazojengwa na msikilizaji.

## 2.7 MKUTANO WA PRAGMATIKI NA TAALUMA YA MITINDO

Njogu na Chimera (1999:384) wanasema, "mtindo ni namna ya kufanya kitu, na ndio unaomtofautisha fanani mmoja na mwingine." Aidha wanasema kuwa, ni huu mtindo unaoufanya ushairi wa mshairi maalumu kutofautiana na mshairi mwingine yeyote.

Osuala (2009:12) anasema, "elimu mitindo ni maelezo na uhakiki wa mabadiliko ya kiisimu katika hali halisi ya matumizi ya lugha." Maoni haya ya yanaonyesha kuwa isimu ni kichangizi kikubwa katika uhakiki wa matumizi ya lugha.

Maoni ya Osuala yanaelekea kukubaliana na maoni ya kimsingi kuhusu elimu mitindo ni nini yaliotolewa na Allan, B. et al (1988) kuwa, " ni tawi la isimu linalochunguza matumizi ya lugha katika miktadha mahususi kwa mkabala wa lugha ya kisanaa na tawi hili linajaribu kuchunguza kanuni zinazopelekea kueleza uteuzi unaofanywa na watu au makundi ya kijamii katika matumizi yao ya lugha."

Katika maendeleo ya kujadili swala la mtindo, Spencer ( 1971:xii) anasema kuwa, " mtindo wa mwandishi unaweza kuchukuliwa kama mtu na ubunifu wake wa kutumia rasilimali za lugha ambazo, wakati, lahaja anayoichagua, utanzu anaouandikia na madhumuni yake yanampa."

Kulingana na Spencer, msanii ana uhuru wa kuteua kutokana na rasilimali pana ya lugha namna ya kuitumia lugha kulingana na utanzu, lahaja au madhumuni ya sanaa yake. Hapa ndipo tunapopata mashiko ya kuchunguza namna Mrisho anavyotumia rasilimali ya lugha ya Kiswahili kwa namna ya kimafumbo ili kumfaidi kupitisha ujumbe wake.

Enkvist et al (1971:12) wanatoa vijelezi sita kuhusu suala la mtindo, wanasema "mtindo ni kama kigae kinachozunguka wazo au usemi uliopo ndani akilini; mtindo ni uteuzi kati ya namna nyinginezo za kutoa kauli; ni kundi nzima la sifa za mtu binafsi; ni ukiukaji wa kaida zilizowekwa; ni kundi nzima la sifa za kijumla na kwamba mtindo ni yale mahusiano kati ya vipengee vya isimu na ambavyo vinatokea katika upana mkubwa wa matini zaidi ya sentensi."

Kutokana na maoni ya Spencer na Enkvist et al, dhana ya pragmatiki na mtindo ni dhana zinazotegemeana na kukamilishana kwa ukaribu sana.

Katika kuweka mkutano huu wa pragmatiki na suala la mtindo wazi, tutatoa maoni ya Dada (2012) katika makala yake alipotumia mtazamo wa kipragmatiki- mitindo kuhakiki kauli ya kifungu cha injili ya Johana 3:16. Anasema hivi, "mwanaelimu mitindo anatumia vyombo na maarifa ya kiisimu katika utekeleza uhakiki wake."

Kwa hivyo, uhakiki wa kimtindo hujihusisha pia kwa kina na sifa za kifonetiki, kileksia, kisemantiki na kipragmatiki katika kazi yoyote ya kisanaa au usemi wowote wa kawaida ambao unachunguzwa kimtindo pamoja na namna msemaji (msanii) anavyohusiana na hadhira yake katika kupitisha ujumbe wake. Na hapa kwa kweli ndipo taaluma ya isimu na fasihi zinapokutana kwa muktadha wa utafiti huu.

Kutokana mjadala wa hapo awali kuhusu mtindo, ni wazi kuwa hakuna mtindo ambao ni bora zaidi kuliko mwingine katika upitishaji wa ujumbe wa msemaji (msanii). Kwamba kila mtindo una utamu wake na ili maana ya kauli kueleweka vizuri lazima mtindo uliotumika uwekwe katika muktadha husika.

Kwa namna fulani upingaji wa kanuni za utaratibu wa ushirikiano husababishwa na matumizi ya mbinu kadha za kifasihi kimtindo, kama vile sitiari, jazanda, kinaya au tashtiti. Maoni haya ndio yanayoufanya mtindo wa Mrisho wa ufumbaji maana kuzua vipengee anuwai vya kushughulikiwa ili kubaini ujumbe utokanao na kauli zake katika mashairi yake teule. Mfichamo ni njia moja tu ya kuangalia maudhui katika nyimbo zake, zipo njia nyinginezo.

## 2.8 HITIMISHO

Katika sura hii, tumeangalia ufafanuzi mbali mbali wa dhana ya pragmatiki na hasa suala la muktadha na maana. Tumeonyesha namna usimbaji wa maana unavyoweza kuzua maana ya mifichamo mbali mbali katika kauli. Isitoshe tumeona umuhimu wa dhana ya mfichamo katika ufafanuzi wa maana katika mazungumzo.

Aidha tumeonyesha mkutano uliopo kati ya pragmatiki na elimu-mitindo katika azma ya kuweka msingi wa mtazamo wa kipragmatiki- mitindo ambao tunautumia katika kuchunguza mashairi teule ya Mrisho. Kwa kuweka wazi dhana hizi muhimu zitatusaidia katika changanua mashairi teule ya *Nikipata Nauli na Sizonje* katika sehemu ifuatayo.

SURA YA TATU

# 3.0 UHAKIKI WA MIFICHAMO KATIKA SHAIRI LA NIKIPATA NAULI

## 3.1 UTANGULIZI

Katika sura hii, tutahakiki shairi la *Nikipata Nauli* kwa kuchunguza namna kauli mbali mbali zinazotumika katika shairi hili zinavyopinga utaratibu wa ushirikiano na hivyo kuzua maana za kimfichamo ambazo zinajenga maudhui anuwai katika shairi hili. Tuangalia namna tamathali mbali mbali za usemi na mbinu za lugha zinavyotumika katika kupinga kanuni za utaratibu wa ushirikiano kisha tuchunguze maudhui yanayojitokeza kutokana na maana za kimfichamo zinazoibuka.

## 3.2 NIKIPATA NAULI

Msanii katika *Nikipata Nauli* amefumba masuala mbali mbali yanayoathiri taifa la Tanzania na mataifa ya Afrika Mashariki kwa jumla kwa kutumia mkakati wa upingaji kanuni za utaratibu wa kimazungumzo. Shairi hili linahusu mhusika ambaye anatamani au kutafuta nauli ili aweze kusafiri hadi mjini ambapo mhusika aitwaye Mjomba ameweka makao. Kama inavyofasirika ni kuwa, Mjomba ni mmoja wa wanakijiji lakini kwa sababu amepewa cheo cha kitaifa inambidi kwenda kuishi mjini karibu na makao makuu ya uongozi. Mjomba, anasahau kurudi kijijini kutimiza ahadi zote alizozitoa kwa wanakijiji ili wamuunge mkono kupewa cheo hicho.

Msimulizi katika shairi hili anatumia tamathali za usemi ambazo zinachora picha ya kujaribu kushawishi mawasiliano ya kisanaa kwa kufuma hisia za msikilizaji kuibuka na maana tofauti tofauti. Kutokana na matumizi hayo ya tamathali za usemi, upingaji wa kanuni mbali mbali za utaratibu wa mazungumzo unaibuka na hivyo usimulizi wa shairi hili unahaishwa zaidi na kufungamanishwa na muktadha wa matukio kuzua maana mbali mbali kwa msikilizaji ambazo matokeo yake ni kujenga maudhui. Kwa kuangalia mifano mbali mbali ifuatayo ya upingaji wa kanuni nne za utaratibu wa mazungumzo, tutaona namna maudhui yanavyojengeka kutokana na maana za kimfichamo.

## 3.3 UPINGAJI WA KANUNI YA UKWELI

Kanuni ya ukweli kwa mujibu wa Grice, inamhitaji msemaji kutoa kauli ambazo ni za kweli. Msemaji asiseme uongo au kutoa kauli ambayo hana ushahidi. Msanii katika shairi hili ametumia kimakusudi baadhi ya kauli ambazo zinapinga kanuni hii ya ukweli. Upingaji huu wa kanuni ya ukweli umefanikishwa kwa matumizi ya tamathali za usemi kama vile sitiari, methali, maswali ya balagha na kejeli. Huu ni mtindo ambao umemsaidia msimulizi katika shairi hili kudhibiti mazungumzo na kumfanya msikilizaji wake kujenga maana za kimfichamo nyingi ambazo zinachangia katika kukuza upana wa kimaudhui wa shairi. Kama vile;

(17) **Pole sana mjomba,** una kibarua kizito kutaka **dunia kuwa kijiji, hongera!**

Kile **kiitikio** cha ***globalisation*** **kimeimbwa vizuri sana japo hakijakaririwa!**

**Nasikia wageni wamefurahi sana kusikia sauti yako**

**Tena wanafurahishwa na ule ubeti wa mwisho uliouongeza**

**Wa mbio zetu kutoka uhuru mpaka hapa tulipo**

Mantiki haituruhusi kukubali kuwa dunia inaweza kuwa kijiji katika hali halisi au kukubali kuwa mtu atakubali kupokea sifa kutokana na kuifanya dunia kuwa kijiji kama vile kauli hii inavyodai. Hapa msanii anatoa kauli ambazo zipo zaidi ya uwezo wake kuzithibitisha.

Hata hivyo, muktadha wa shairi la *Nikipata Nauli* unatufanya kuchukulia maana ya mfichamo ya kauli ***pole sana mjomba, una kibarua kizito kutaka dunia kuwa kijiji, hongera!*** Msimulizi anajaribu kumtia moyo mgombea wa wadhifa wa uongozi kwa kuwa ana mipango mizuri mizito na ahadi nzuri za kujenga taifa kwa kuwa na mradi wa kufanya taifa liwe taifa la kiteknolojia. Suala la maendeleo ya kiteknolojia linajitokeza.

Kwa namna nyingine, inawezekana kuwa msimulizi anamkejeli kiongozi huyu kwa kuwa na ahadi nzito za uongo ili kuwahadaa wapiga kura kumchagua katika wadhifa anaouwania. Hii inajitokeza kuwa kauli ya kikejeli na hivyo inapinga kanuni ya ukweli katika utaratibu wa mazungumzo. Maudhui ya tamaa ya uongozi yanajitokeza. Yaani pale viongozi wanaotaka kuingia madarakani wanawaahidi wapiga kura kitu chochote hata kile wasicho na uwezo wa kukifanya ili wapigigwe kura. Hili linajengwa zaidi katika kauli inayofuata kwamba; ***kiitikio cha globalisation kiliimbwa***

***vizuri sana japo hakijakaririwa.*** Ule mfichamo wa maana kuwa kauli ya kwanza ni uongo wa viongozi ili kuingia madarakani unadhibitika katika kauli hii kwamba, viongozi waliimba na kudai maendeleo ya kiteknolojia watakapoingia madarakani, lakini walipoingia uongozini walisahau kwa kuwa hawakuwa wamakariri walichokisema au walichowaahidi wananchi. Kwa maana chochote kisichokaririwa, husahaulika haraka.

Kauli, ***nasikia wageni wamefurahi kusikia sauti yako,*** ina maana ya kuwa kimsingi wageni waliohudhuria hotuba ya kiongozi walifurahikia yale aliyoyasema.

Muktadha wa kauli hii unatufanya kuibuka na maana nyingine kuwa, kauli hii ni ya kinaya ambayo inapinga kanuni za utaratibu wa kimazungumzo. Wageni hawa wanafurahishwa na ahadi butu za viongozi wa Afrika pamoja na njama zao za kuwapora wananchi wa Afrika kwa kutumia viongozi hawa. Maana hii ya kimfichamo inaibuka kutokana na kauli inayofuata kwamba, ***tena walifurahishwa na ubeti uliouongeza, wa mbio zetu tangu uhuru hadi tulipo.*** Maana ya kimfichamo inayojitokeza ni kuwa wageni hapa ni mataifa ya kigeni ambayo yanashabikia uongozi mbaya wa mataifa yanayoendelea ya ulimwengu wa tatu kwa faida zao za kibinafsi. Wanafurahia kusikia sauti ya kiongozi huyu kwa kuwa, kutokana na ahadi za kiteknolojia alizozitoa watapata mikataba ya kuuza teknolojia zao hata kama ni miradi bubu ambao hautatimika. Maudhui ya ukoloni mamboleo yanajengeka kutokana na upingaji huu wa kanuni za ushirikiano wa kimazungumzo.

(18) **Bora kujenga daraja, kuliko ukuta**

Msimulizi anapotoa kauli hii anavunja mawasiliano kati yake na msikilizaji wake kwa kutumia tamathali ya usemi ya sitiari. Kujenga daraja kuliko ukuta ni usemi unaozua maswali mengi ya maana unapoambatanishwa na muktadha wa shairi lenyewe. Sitiari za *daraja* na *ukuta* zinapinga kanuni za utaratibu wa ushirikiano ambao unahitajika. Hivyo basi msikilizaji ataunda maana nyingine za usemi huu kwa kuhusisha kauli hii na muktadha husika. Daraja ni sitiari ya ushirikiano, utangamano na umoja ilhali ukuta ni sitiari ya utengano pamoja na ubinafsi. Maana ya kimfichamo ya kauli hii ni kuwa, msimulizi anahimiza kiongozi kufanya kila juhudi kurahisisha utangamano wake na raia waliompigia kura badala ya kuwapuuza, maana ukuta huzuia mtu kupenya au ni ishara ya kujitenga na watu na kuishi katika hali ya kipekee. Upingaji huu wa kanuni ya ukweli katika kauli hii unatufanya kupata maudhui ya ubinafsi wa viongozi wanapofika madarakani.

Kwamba siku zote viongozi hawa husahau ahadi na kuishia kuwa wabinafsi na kuwapuuza raia waliowateua.

Kwa upande mwingine kauli hii ina maana ya kuwa, msimulizi anamuhimiza kiongozi awe sifa njema ya kuwaunganisha wananchi na wala si kuwasambaratisha kimipaka. Maudhui ya umoja, ushirikiano pamoja na ubinafsi wa viongozi yanajitokeza kutokana na upingaji huu wa kanuni ya ukweli.

(19) **Kufumbatia maji kama jiwe ni ujinga**

Kauli hii vile vile inapinga kanuni ya ukweli ya utaratibu wa ushirikiano kwa kujenga taswira ya mfumbato wa maji. Katika hali halisi mtu hawezi kufumbatia maji kama atakavyofumbata jiwe. Mfichamo wa kauli hii ni kuwa wananchi wameambulia patupu kutokana na viongozi kutotimiza ahadi walizozitoa na hivi sasa wanaona wamedhulimiwa na kudanganyika. Usemi huu ni wa kuonyesha kukata tamaa walio nako wananchi wengi ambao walitamani kuona ahadi za viongozi wao zikitimika kwa nchi yao.Maudhui ya mapuuza ya viongozi, ubinafsi wa viongozi pamoja na hali ya ukataji tamaa ya wananchi yanasisitizwa katika kauli hii.

(20) **Ukicheka na nyani utavuna mabua mjomba!**

Hii ni kauli nyingine ambayo inapinga kanuni ya ukweli kwa kutumia taashira ili kujenga maana ya kimfichamo. Uhalisi wa kauli hii ni uhusiano wa nyani na mahindi. Kwamba nyani anapenda mahindi ambayo hayajakomaa sana kwa hivyo mkulima lazima awe makini kuyalinda mahindi yake dhidi ya nyani hadi yakomae na kuvunwa. Katika muktadha wa shairi hili, wananchi wamechoka kuchezewa na viongozi na hasa rasilimali zao zinavyoporwa. Kwa hivyo hii ni kauli ya kiuanaharakati ili kuwazindua wananchi wengine ambao bado hawajapata ukweli kuwa hazina ya nchi yao inaporwa na huenda wakakosa maendeleo yoyote kama hawatasimama kidete kulinda hazina yao ya nchi kwa kupambana na wezi wa rasilimali za nchi. Suala la uanaharakati na uporaji wa mali ya umma linajengwa na upingaji huu wa kanuni ya ukweli.

Msimulizi pia anatoa kauli ya dhihaka anaposema;

(21) **Mtoto wa nyoka hafundishwi kuuma**

Kulingana na muktadha wa shairi hili hakuna ukweli kuwa kuna mtoto wa nyoka na mafundisho ya kuuma, kwa hivyo kauli hii imepinga kanuni ya ukweli. Maana ya kimfichamo inayoibuka ni

kuwa viongozi katika mfumo wa serikali husika wamezoea kuiba mali au dhuluma walizonazo za kutojali wananchi, mpaka wale viongozi wageni wanaoteuliwa pia wanaishia kufuata mkondo huo bila mafunzo yoyote. Kwa hivyo maana iliyofichama hapa ni kuwa viongozi wote hawaonyeshi matumaini ya uongozi mzuri, hata wale viongozi wageni wanapoingia madarakani hufuata mkondo wa viongozi waliowatangulia. Hii ndio sababu inamfanya msimulizi kuongeza kwa kusema *mbwa hafi kwa kuona uvuko.* Mfichamo wake ni kuwa mbwa ni sitiari ya watu walio na sifa mbaya za ulaji mbaya wa vyakula visivyo safi. Kwa maana hiyo wanapopora mali ya umma kupitia ufisadi hawashtuki kwa maana uozo huo hauwaletei majuto yoyote moyoni.Maudhui ya ufisadi na uongozi mbaya yanajengeka kutokana na maana ya mifichamo ya kauli hii.

(22) **Tabia ni kama ngozi huwezi kuibadili**

Kauli hii vile vile imepinga kanuni ya ukweli kwa kuhusisha tabia na ngozi. Tashbihi kama tamathali ya usemi imetumika na msanii kupinga utaratibu wa mazungumzo. Hapa msikilizaji anaishia kijenga maana za kimfichamo kuhusu namna tabia ilivyo ngozi kulingana na mkutadha wa shairi hili. Maana zinazojengeka ni kuwa, viongozi walio na hulka za kuiba mali ya umma au kutoa ahadi za uongo hawawezi kukoma tabia hiyo. Wataonekana kuwa wazuri kwa muda mfupi tu wa uchaguzi, lakini muda huo unapokwisha wanarejea kuwa wale wale viongozi fisadi,katili, wadanganyifu, wezi wa mali ya umma na uozo mwingi katika jamii.

Pia kauli hii inazua maana nyingine ya kusisitiza maudhui ya ukataji tamaa. Kwamba, japo wananchi wanaelewa kuwa viongozi hawa ni wadanganyifu, wanawachagua tu kwa kuwa hawana kingine cha kufanya kwa maana tabia yao wote imekuwa sawa. Hawawezi kubadilishwa na msukumo wowote. Hivi kwamba wanasiasa wote wanafanana kwa ubinafsi wao, labda kile ambacho kitawatofautisha ni aina au kiwango cha ubinafsi.

Msimulizi aidha anapoendelea kuhoji tabia za viongozi katika jamii hii, anatumia maswali ya balagha kudhihaki msamaha wa viongozi. Anasema;

(23) Eti **wanaomba samahani,**

**Watarudisha uhai wa waliopotea kwa uzembe wao?**

Kauli hizi katika muktadha wa wimbo huu zinapinga kanuni ya ukweli. Haiwezekani uhai wa watu waliokufa kurudishwa. Vile vile hakuna ukweli wa watu kupeana masikio ya wengine kama zawadi. Msikilizaji analazimika kujenga mfichamo wa yale yaliyosemwa katika kauli hizi.

Kulingana na muktadha wa kauli hizi, suala la mapuuza ya viongozi katika taifa linajiri zaidi. Uzembe na kutojali wa viongozi unasababisha maafa mengi ya wananchi. Isitoshe viongozi hawajawajibika katika kuangazia masilahi muhimu ya wananchi, ndio maana kunatokea vifo.

(24) **Watawanyang'anya waliowapa masikio yetu kama zawadi?**

Viongozi wanaotajwa hapa aidha wamedinda kusikiliza lalama na matatizo ya wananchi wanaoteseka. Badala yake yamewapa jukumu hilo vikaragosi wao ambao hawajali kusikiliza kamwe.

Kwa upande mwingine, mfichamo wa kauli hii ni kuwa, wananchi wamenyimwa haki ya kutumia na kupata mahitaji ya kimsingi kama ilivyo kumnyanganya binadamu masikio yake. Badala yake rasilimali zilizotengewa matumizi ya mahitaji ya kimsingi ya umma kama vile shule, afya na chakula zimepewa marafiki na jamaa za viongozi kama zawadi.

Suala la matumizi mabaya ya rasilimali za nchi linajitokeza zaidi katika muktadha wa wimbo huu pale msimilizi anapotoa kauli namna viongozzi wanavyotumia uwezo wao kuwakandamiza wananchi. Anasema:

(25) **Migodi sita! Yote kwangu**

**Hekari mia moja! Najiandaa kustaafu nipate sehemu ya kupumzika**

**Mazihala je? Aah, aliyemwoa mtoto wa mjomba wangu, kakake na mamangu nikampa zawadi**

Msimulizi anajenga taswira katika picha ya msikilizaji kuhusu namna viongozi hawa wanavyogawa rasilimali za nchi kibinafsi kwa nia ya kujifurahisha wenyewe. Na kwa sababu masikio ya kusikiliza wananchi yalishapeanwa, viongozi hawa hawasikii lalama na mateso ya wananchi na hakuna ishara kuwa wataweza kusikia.

Maudhui ya mapuuza pamoja na matumizi mabaya ya rasilimali za umma yanajengwa kutokana na mfichamo wa kauli hizi ambazo zimepinga kanuni ya ukweli.

(26) **Inauma sana kugawa malalio yetu kama zawadi, mjomba**

Katika kauli hii neno *malalio* limetumika kisitiari. Matumizi ya sitiari yanapinga kanuni ya ukweli katika mazunguzo. Katika muktadha wa shairi hili, msikilizaji anahitajika kujenga mfichamo ili kuelewa msimulizi. Mfichamo unaojitokeza kulingana na muktadha wa wimbo huu ni kuwa, malalio ni ardhi ya taifa hili. Viongozi katika taifa hili wanagawa ardhi ya nchi kwa manufaa yao wenyewe bila kujali uwepo wa wananchi wengi maskini. Maudhui ya ubinafsi na uongozi mbaya yanasisitizwa kwa upingaji huu wa kanuni kwa namna ya kutumia sitiara *malalio*.

## 3.4 UPINGAJI WA KANUNI YA IDADI

Msimulizi katika shairi hili anatoa baadhi ya kauli ambazo zinapinga kanuni ya idadi ya utaratibu wa ushirikiano katika mazungumzo. Kanuni ya idadi inamhitaji mzungumzaji kutoa kauli ambazo zinatoa mchango unaohitajika tu katika mazungumzo husika. Aidha, mzungumzaji asifanye mchango wake kuwa na habari zaidi ya yale yanayohitajika katika mazungumzo husika au asifanye mchango wake kuwa finyu sana. Pale mzungumzaji anapobana mchango wake au kutoa habari zaidi ya yale yanayotakikana katika mazungumzo yake huwa ana sababu za kufanya hivyo kimakusudi.

Msanii Mpoto katika shairi hili la *Nikipata Nauli*, ametumia tamathali mbali mbali zinazozua upingaji huu wa kanuni ya idadi katika mazungumzo. Kwa mfano, kwa matumizi ya dhihaka na uradidi katika baadhi ya kauli zake, msanii amefaulu katika kumpa msikilizaji sababu za kujenga maana za kimfichamo za kauli hizo.

(27) Watawanyanganya waliowapa masikio yetu kama **zawadi?**

Mazihala je? Aah, aliyemwoa mtoto wa mjomba wangu, kakake na mamangu nikampa **zawadi**

Inauma sana kugawa malalio yetu kama **zawadi**

Urudiaji wa neno **zawadi** katika kauli hizi katika shairi hili unapinga kanuni ya idadi katika mazungumzo. Athari ya neno **zawadi** katika kauli ya kwanza ni tofauti ile ya matumizi ya neno hilo katika kauli zinazofuata. Katika kauli zinazofuata kauli ya kwanza neno hili hata

lisingekuwepo bado muktadha wa shairi ungetosha kueleta ushirikiano katika mazungumzo lakini msanii anapinga kanuni ya idadi kwa kutoa habari zaidi ya ile anayofaa kutoa katika muktadha huu.

Makusudi ya kurudia neno hili kimaudhui ni kusisitiza namna wananchi walivyokereka na tabia za kutojali za viongozi ambao ni walafi na hawawajibikii namna wanavyotumia rasilimali za nchi. Kutoa rasilimali za nchi kama zawadi ni kutumia mali ya umma kuholela bila kujali hatima ya nchi na wajibu waliopewa viongozi kulinda rasilimali hizo. Aidha neno **zawadi** katika kauli hizi linaleta mfichamo wa dhana ya kinasaba katika uongozi hivi kwamba jamaa na marafiki wa viongozi walio madarakani wainaishia kufaidi rasilimali za nchi bila kufanyia kazi yoyote.

(28) Mjomba, *life is not a rehersal,* ***it is a performance!***

Kanuni ya idadi inamhitaji msemaji kutotoa mchango zaidi ya ule unaohitajika katika mazingira ya mazungumzo. Katika mazungumzo, kusema *life is not a rehersal* ni sawa na kusema *it is a perfomance.* Msimulizi hivyo basi anaongeza kauli, ***it is a performance!*** Hapa msanii anapinga kanuni ya idadi kimakusudi ili kuzua maana za kuimaanisho.

Maana inayoibuka hapa ni kuwa wananchi wamezinduka na wanahitaji viongozi wao wawajibike katika kutekeleza majukumu yao kwa haki. Kwa upande mwingine, kauli hii ni ishara ya hisia kali za mateso wanayoyapitia wananchi kutokana na mapuuza ya viongozi wao na huu ni wito wa suluhu ya haraka kutafutwa ili kurekebisha hali ilivyo. Maudhui ya uanaharakati yanajengeka kutokana na upingaji kanuni katika kauli hii.

(29) Hofu yangu, siwaoni kwenye nyama siku hizi

Hata lile la kulala limepungua

Mawili,

Wanasoma sana miswada au kwa kuwa *live* runingani **wanauza sura**

Kauli ya kuuza sura ni usemi wa dhihaka. Kauli hii imebana maelezo ya sifa za viongozi walivyo wazembe na walafi. Katika mazungumzo msikilizaji angejiuliza ni vipi viongozi hawa wanauza sura runingani lakini kwa sababu ya muktadha, tunapata mfichamo kuwa viongozi hawa wanaenda katika vituo vya runinga kushiriki katika mijadala ya kitaifa ambapo hawana sera maalumu ya kufaidi au chochote cha kuwatia moyo wananchi kuhusu nchi yao. Aidha uuzaji sura

unaleta mfichamo wa kuwepo kwa viongozi ambao mara nyingi wanatumia vyombo vya habari vibaya kwa sababu zao za kibinafsi kama vile kuficha uzembe wao wa kulala bungeni au ulafi wao. Hii ndio maana msimulizi anasema kuwa, hawaonekani kwenye nyama siku hizi, hata kulala kwao bungeni kumepungua.

Mfichamo mwingine hapa ni kwamba, wananchi wamekata tamaa kiwango cha kuwaona viongozi kutowajali kwa hali yoyote ile. Sifa zao zinapodhaniwa kuwa ni afadhali kidogo kuacha kulala bungeni, ndipo wanapopatikana kuuza sura runingani. Hii ni ishara ya umma uliokata tamaa kuhusu vingozi wake.

(30) Tazama maisha yetu, **utadhani mchezo wa kuigiza!**

Kulingana na maoni ya Grice, kanuni ya idadi inamtaka mzungumzaji aseme habari yote inayohitajika kwa msikilizaji. Pale kanuni hii inapopingwa kimakusudi, mfichamo wa kimazungumzo hujengeka kwa msikilizaji. Katika shairi hili msanii Mrisho ndiye mzungumzaji na msomaji au msikilizaji wamnakamilisha mfumo wa kimazungumzo.

Basi msanii anapotoa kauli hii hapo juu, msikilizaji hana budi ila kujenga mfichamo kwa kuwa kauli hii ni ya kidhihaka na haitoi habari za kutosha kuelezea kile anachotaka kukisema mzungumzaji. Msikilizaji atahitajika kujenga mfichamo kutokana na kichochezi cha muktadha pamoja na uelewa wake wa mchezo wa kuigiza.

Mfichamo unaojengeka hapa ni kuwa, wananchi wanahofia maisha yao kutokana na hali duni ya kuishi na kuwepo na viongozi ambao hawajali na kutilia maanani masilahi ya mwanachi. Maudhui ya uongozi mbaya yanasisitizwa katika kauli hii kwa kuonyesha namna viongozi wanavyokwa kikwazo kikuu kwa wananchi kuishi maisha ya kiuhalisia ya binadamu yeyote. Isitoshe, wananchi wamezinduka, kwa kuwa wameelewa hali yao ndio maana wanaweza kuyaona maisha wanayoyaishi kuwa si maisha halisi wanayofaa kuishi katika taifa huru na lenye serikali inayowajibika.

(31) ***Please*, tafadhali!** Wacha maagizo mlangoni, maana siku hizi wanataka sifa kweli, hawachagui pa kupiga

Msimulizi katika shairi hili anataka kuenda kumwona mjomba jijini atakapoata nauli ili amweleze matatizo wanayokumbana nayo kama wananchi vijijini. Katika kauli yake ya mwisho anamrai kwa

upole kuwa awaachie maagizo walinzi wa lango la ofisi yake kuwa anakuja kwa kuwa siku hizi walinzi hao hupata sifa kwa kupiga na kuua wanachi kiholela.

Maneno *please* na *tafadhali* kimsingi yana maana moja ya kisemantiki. Kwa hivyo kuyatumia maneno haya moja kwa moja katika mfuatano wa kauli moja ni kutoa habari zaidi yale anayohitajika kutoa msemaji. Katika urudiaji msimulizi amepinga kanuni ya idadi katika mazungumzo haya.

Mfichamo unaojengeka hapa ni kuwa msimulizi anahofia hata vyombo vya umma ambavyo vinatumika vibaya kuwafurahisha viongozi wachahe. Polisi kama chombo cha serikali kinatumika kuwakandamiza wananchi walio na ari ya kuona mabadiliko katika nchi yao. Polisi wanatumika katika kuwanyamazisha wananchi wanaoleta malalamishi katika ofisi za serikali.

Aidha upingaji huu unajenga mfichamo wa dhuluma na mateso wanayopitia wananchi mikononi wa polisi. Kwa kurudia neno *tafadhali* ni ishara hisia nzito anazozitoa mwananchi kutokana na hofu ya vitendo vya kiukatili vya polisi maana hawabagui pa kupiga. Jukumu kuu la polisi katika taifa ni kulinda usalama, lakini pale majukumu yanapobadilika kwa kuwapiga kiholela wananchi ili kuwafurahisha viongozi, dhima ya vyombo vya usalama katika taifa husika inapotea. Isitoshe, kauli hii inaweza kuleta maana ya kuwa, kwa kutumia neno *please,* msimulizi ana matumaini kuwa atawafikia viongozi/watu wa tabaka la juu ili waoate kuelewa mateso wanyonge wanapitia katika jamii.

## 3.5 UPINGAJI WA KANUNI YA NAMNA

Kanuni hii inamhitaji msemaji kutoa kauli zake kwa njia inayoeleweka zaidi. Vijikanuni vyake vinadai kuwa, msemaji aseme mambo kwa uwazi wa kueleweka aidha atoe kauli kwa kifupi bila kujirudia rudia.

(32) **Maana tabia ni kama ngozi, hauwezi kuibadili**

**Na mtoto wa nyoka hafundishwi kuuma**

**Ukicheka na nyani utavuna mabua mjomba!**

**Masikini mtu kwao, ugeni si kitu chema**

**Msimu wowote kuanza upya si ubaya,**

Kauli hizi zinazofuatana katika ubeti huu zinapinga kijikanuni cha kusema mambo kwa wazi. Msikilizaji analazimika kujenga mfichamo pale anapopokea kauli hizi kwa kuwa namna zilivyotolewa na msemaji si ya wazi. Mfichamo unaotokana na mfuatano wa kauli hizi ni kuwa wananchi wanashangaa namna viongozi waliowachagua wanakuwa wageni kwao kwa kuwa wamepotelea jijini na kuwa hawana namna nyingine ya kujinusuru ila tu kuanza upya kuandaa viongozi wengine ambao watawawakilisha vizuri msimu ufuatao maana waliowachagua msimu huu wamefeli.

(34) **Maana lake mtu halimtapishi**

**Lakini kufumbatia maji kama jiwe ni ujinga**

Kauli hii pia inapinga kijikanuni cha uwazi kuwa kuwa kauli mbili zinafuatana ambazo zinazua utata kwa uelewekaji kwa msikilizaji. Hapa msanii ametumia methali na msemo mtawaliwa bila kuweka wazi ujumbe.

Mfichamo unaojengeka hapa ni kuwa, msimulizi anaelekea kutoa ujumbe kuwa wananchi wanatosheka kuwa kiongozi anayewadhulumu anatokea kijijini mwao na hivyo hawangependa kumsema vibaya. Hata hivyo, msimulizi anatahadharisha wananchi dhidi ya kujitia moyo kutokana na ukweli kuwa kiongozi huyo anatoka kijijini mwao na kuona sura yake ya ahadi za uongo ambazo hazijatekelezwa na hakuna matumaini yazo kutekelezwa. Kimsingi msimulizi anawazindua wananchi wamwangalie kiongozi huyo kama mtu anayechezea rasilimali zao na wasipogutuka mapema huenda akafilisisha taifa wakabaki daima masikini.

(35) ***Please*, tafadhali! Wacha maagizo mlangoni, maana siku hizi wanataka sifa kweli, hawachagui pa kupiga**

Kijikanuni kimojawapo katika kanuni ya namna ni kusema mambo kwa kifupi. Kulingana na kauli hii, msimulizi hangekuwa haja ya kurudia kusema *tafadhali* baada ya kusema *please.* Hapa kijikanuni hiki cha namna kinapingwa na hivyo msikilizaji atajenga mfichamo kauli hii inapomfikia.

Mfichamo unaojengeka kutokana na urudiaji huu ni kuwa msimulizi ananuia kuonyesha kiwango ambavyo vyombo vya umma vinatumiwa na viongozi kuwatesa na kuwaangaisha wananchi wanaotaufuta huduma za serikali. Vile vile ni hisia kuonyesha namna vyombo vya serikali vinavyofaa kuwatumikia wananchi vilivyobinafsishwa kutumikia viongozi. Kwa kuwa ukatili wa polisi unatoka na kutaka kusifiwa na viongozi kwa kuwapiga wananchi ambao wanafaa kuwalinda dhidi ya dhuluma hizo.

## 3.6 UPINGAJI WA KANUNI YA UHUSIANO

Kanuni hii inamhitaji msemaji katika mazungumzo kutoa mchango wake kuhusiana na muktadha wa mazungumzo. Chochote ambacho kinachosemwa nje ya mazingira ya mazungumzo huwa kinapinga kanuni hii ya uhusiano.

(36) **Na mtoto wa nyoka hafundishwi kuuma**

Kulingana na mazingira ya shairi hili, swala la mtoto wa nyoka kutofundishwa kuuma linatoka nje ya muktadha. Hivyo basi mfichamo utakaojengeka kwa msikilizaji ni kuwa viongoz wapya kila wanapoingia uongozini huwa hawafundishwi kuiba mali ya umma maana hii ni mada inayozungumzwa kila siku hadi jamii pamoja na vizazi vinavyozaliwa vinapata tabia hii kama utamaduni wa kurithishwa. Pale kiongozi mpya anapoingia madarakani akitarajiwa kuleta mabadiliko anapata ugumu wa kufanya hivyo kwa kuwa tabia ya ubinafsi imejengeka katika jamii hii kiasi cha kwamba msimulizi katika shairi hili hana matumaini ya kuibadilisha. Hii ndio sababu anataka nauli ili asafiri moja kwa moja hadi ofisini mwa kiongozi kumweleza matatizo ya kijiji chao kwa kuwa ana hakika kiongozi huyo hatakumbuka ahadi alizozitoa wakati wa kampeni.

(37) **Ukicheka na nyani utavuna mabua mjomba!**

Suala la kucheka na nyani na kuvuna mabua ni nje ya mkutadha wa shairi hili. Msanii anatumia taswira hii ambayo inamchochea akili msikilizaji kujenga mfichamo wa kauli yenyewe. Maudhui ya wito wa kuzinduka yanajengwa katika mfichamo wa kauli hii. Wananchi wanazinduliwa kutetea haki ya kutumia rasilimali za nchi yao kwa kuwa viongozi walio madarakani wanaonekana kuwa walafi na wenye tamaa ya mali.

## 3.7 HITIMISHO

Katika sura hii tumejadili namna kauli mbali mbali zinavyopinga kanuni ya ukweli, udadi, namna na uhusiano katika mzumngumzo. Pia tumechunguza tamathali mbali mbali za kiusemi zilizotumika na msanii katika shairi hili kupinga kanuni za utaratibu wa ushirikiano. Vile vile tumechunguza mfichamo unaojengeka kutokana na kila mojawapo wa kauli zilizopinga kanuni za utaratibu wa kimazungumzo kisha tukaangalia namna mfichamo huo unavyochangia katika kuimarisha maudhui mbali mbali katika shairi hili.

# SURA YA NNE

## 4.0 UHAKIKI WA MIFICHAMO KATIKA SHAIRI LA SIZONJE

### 4.1 UTANGULIZI

Katika sura hii tutahakiki upingaji wa kanuni za utaratibu wa kimazungumzo kwa kuchunguza kauli mbali mbali zinazotumika katika shairi hili la *Sizonje* ambazo zinapinga utaratibu wa kimazungumzo. Madhumuni yetu ni kuchunguza namna kauli zinazopinga utaratibu wa ushirikiano zinavyozua maana mbali mbali za kimfichamo ambazo zinajenga maudhui anuwai katika shairi hili. Pia tutaangalia namna tamathali mbali mbali za usemi na mbinu za lugha zinavyotumika katika kupinga kanuni za utaratibu wa ushirikiano kisha tuchunguze maudhui yanayojitokeza kutokana na maana za kimfichamo zinazoibuka.

### 4.2 SIZONJE

Katika shairi hili, msanii anafumba uovu na ufisadi unaotokea katika mataifa ya Afrika Mashariki kwa jumla katika hafla ya kuwakaribisha viongozi wapya madarakani. Ni shughuli inayofanyika kwa haja ya kupokezana uongozi na kiongozi mgeni kuhamazishwa kuhusu taasisi au ofisi anayoingia kuiongoza.

Katika shairi hili, msimulizi anatoa kauli zinazopinga kanuni za utaratibu wa kimazungumzo kwa namna anavyowasawiri wenyeji wanaomkaribisha kiongozi mgeni- Sizonje. Katika makaribisho hayo, Sizonje, anaonyeshwa sehemu mbali mbali za nyumba pa moja ma mazingira ya nyumba hiyo.

Kama inavyoonekana , Sizonje anakaribishwa kwa nyumba ambayo atairithi kwa muda. Hii ndio maana anafaa kuhamazishwa vilivyo kuhusu taratibu mbali mbali za nyumba hiyo. Msimulizi katika shairi hili anafanya kazi ya kumwonyesha Sizonje maeneo mbali mbali, kwa mfano, shimo la taka, sebuleni, jikoni, uani na msalani. Isitoshe, msimulizi anamweleza Sizonje kuhusu makaburi yaliopo uani mwa nyumba ambayo hayahitaji kufukuliwa. Kwa jumla hili ni shairi linaloshughulikia maswala mbali mbali yanaliyowapata wenyeji ambao wana matumaini makubwa kwa mgeni Sizonje, kuwa atawasaidia kutatua matatizo yao.

Kutokana na masimulizi ya msanii, kanuni za utaratibu wa ushirikiano zinapingwa kwa kiasi fulani ili kufanikisha ufumbaji wa maana katika shairi hili. Hali hii inasababishwa na matumizi ya mbinu mbali mbali za lugha ambazo ni viungo muhimu katika upingaji wa kanuni hizi. Maana za kimfichamo zinazoibuka katika kauli hizi zinachangia katika kujenga maudhui anuwai yanayojitokeza katika shairi hili. Kama vile uzalendo, utaifa, ufisadi, uongozi wa kinasaba miongoni mwa maudhui mengine. Kwa kuangalia mifano mbali mbali kutoka kwa shairi hili, tutachunguza namna mfichamo unaoibuka kutokana na upingaji wa kanuni za utaratibu wa ushirikiano wa kimazungumzo, unavyojenga maudhui mbali mbali katika shairi hili.

## 4.3 UPINGAJI WA KANUNI YA UKWELI

Mihimili ya kanuni ya ukweli katika utaratibu wa ushirikiano wa kimazungumzo inamhitaji mzungumzaji kusema mambo ambayo ni ya kweli na ambayo msemaji huyo anaweza kuyathibitisha kuwa ya kweli. Isitoshe kauli anazozitoa msemaji ziwe na ushahidi wa kweli. Msanii katika shairi hili ametumia kauli katika masimulizi yake ambazo zinapinga ukweli katika utaratibu wa ushirikiano wa kimazungumzo.

(38) **Sizonje hii ndio nyumba yetu, milango ipo wanapita madirishani.**

Msimulizi anapinga kanuni ya ukweli katika kauli hii, kwa kuwa hakuna ushahidi kuwa pana uwezekano wa milango kuwepo kwa nyumba kisha watu wakapitia madirishani. Usemi huu basi unatupa haja ya kujenga mfichamo wake kulingana na muktadha wa masimulizi haya.

Mfichamo unaojitokeza hapa ni kuwa, nyumba inayorejelewa katika kauli hii ni taifa, nchi au taasisi fulani. Msanii hapa anapinga kanuni ya ukweli kwa matumizi ya sitiari. Nyumba ni sitiari ya taifa, taasisi ya serikali au shirika lolote la umma. Isitoshe, msanii anasisitiza sitiari katika kauli hii kwa kudai kuwa *"watu wanapita madirishani hali milango ipo"*. Mfichamo katika kauli hii ni kuwa, kunao mfumo na utaratibu mwafaka uliowekwa wa kufanya mambo kwa njia nzuri yenye ustaarabu lakini watu hapa wamezoea kutumia milango ya nyuma na njia za mkato. Kutokana na mfichamo huu, maudhui ya ufisadi na namna watu katika taifa hili walivyo na tamaa ya kufanya mambo kwa njia za mkato, yanajengeka.

**(39) Kwani, makaburi yaliyofukuliwa lazima yazikwe upya?**

Kauli hii ni swali la balagha ambalo linazua maana nyingi kutokana na muktadha wa shairi hili. Katika kauli hii, msimulizi anapinga kanuni ya ukweli kwa kuuliza mambo ambayo hakika hayawezi kutendeka katika hali halisi kama vile kufukua makaburi na kuyazika upya.

Msimulizi katika shairi hili, kimsingi anamkaribisha kiongozi mgeni katika nchi au viongozi wapya katika utawala fulani. Mwanzoni kabla ya kauli hii anadai kuwa, hii nchi anayomkaribisha mgeni kwayo ni nchi iliyosheheni na kuwaficha wezi wengi pamoja na kuwa kitovu cha kuwatengenezea wezi. Mfichamo unaotokana na swali hili la balagha ni kuwa, mhusika Sizonje anatahadharishwa kufukua sakata za wizi zilizosahaulika. Kwa upande mwingine, msimulizi ana haja ya kumweleza Sizonje kuwa katika nchi hii, kuna maovu mengi yanayotendeka hadharani-makaburi yaliyofukuliwa. Kwa kumwelezea hivi anasisitiza kwa kumwambia kuwa asiyafungie jicho maovu hayo. Kwamba anapoingia madarakani Sizonje, ahakikishe kuwa uozo huu usisahauliwe kwa kuzikwa bali huwekwe hadharani na kurekebishwa.

**(39) Nyumba hii Sizonje ina vyumba vinne**

**Vitatu havifunguki, kimoja hakina mlango**

Kauli hii imepinga kanuni ya ukweli kwa namna mtumizi anavyotumia sitiari kuficha dhana halisi vyumba vinne katika nyumba hii kuu. Kama tulivyokwisha kutaja hapo awali ni kuwa, sitiari ya nyumba ni taifa au taasisi fulani ya umma. Mwandishi anapotoa kauli kuhusu nyumba hii kuwa na vyumba vinne, tunalazimika kujenga mfichamo kuhusu vyumba hivi.

Mfichamo unaojitokeza hapa ni kuwa katika taifa hili kuna idara au sekta nne muhimu ambapo tatu zimekwama kabisa na ile iliyobaki moja inafuja madhali haina kidhibiti chochote. Msimulizi katika kauli hii anadai kuwa, *waliketi barazani* nje ya nyumba hii. Hapa kuna mfichamo kuwa, katika shughuli muhimu za taifa wananchi hawahusishwi na hivyo wanabaki wakisubiri maendeleo ambayo hayaji pamoja na kwamba hakuna matumaini ya kuwepo kwa maendeleo. Hii inaashiria utepetevu wa viongozi katika kutimiza majukumu muhimu kwa taifa.

**(40) Wenyeji wanalala sebuleni na walishazoea**

Kauli hii pia inapinga kanuni ya ukweli kwa namna inavyozua mifichamo ya kimaana. Ukweli wa kauli kuwa wenyeji katika nyumba hii wanalala sebuleni unatiliwa shaka na hivyo kuzua

mfichamo. Wageni wapo, wamejifungia chumbani na wanazungumza lugha ambayo haieleweki na wenyeji. Ni kinaya kuwa wenyeji hawana fursa ya kulala vyumba vya kulala ilhali wageni ndio wamepewa kipaumbele katika vyumba hivyo.

Mfichamo hapa ni kuwa, wananchi katika taifa hili hawapewi nafasi katika shughuli za nchi yao ilhali wageni wamepewa nafasi hizo. Kwa namna hii msimulizi anafaulu kuzungumzia maudhui ya mapuuza ya viongozi kwa wananchi na ukoloni mamboleo katika mataifa mengi ya Afrika.

Isitoshe, ishara ya kuwa wageni waliopo ndani hawazungumzi Kiswahili, inatilia maanani namna raia wa mataifa ya nje walivyomiliki shughuli za mataifa ya Afrika huku wenyeji wakiteseka katika upweke na umasikini. **Ijapokuwa kina watu ndani, na hawaongei Kiswahili**. Kauli hii inasisitiza maudhui ya ukoloni mamboleo na mataifa yaliyoendelea yalivyochukua nafsi ya kutoendelea kiuchumi kwa baadhi ya mataifa ya Afrika ili kuwadhulumu.

**(41) Wanashangaa, mbona ghafla?**

Hili ni swali la balagha ambalo linapinga kanuni ya ukweli katika utaratibu wa mazungumzo. Katika shairi hili, mhusika Sizonje, anaonekana kuwa kiongozi ambaye atakuja kulikomboa taifa hili kutokana na matatizo yanayolikumba. Msimulizi anatoa kauli hii kwa kejeli, kuonyesha namna viongozi wenyeji wa taasisi mbali mbali katika taifa hili walivyotiwa kiwewe kwa mjo wa mgeni Sizonje. Kimsingi ni kuwa, viongozi wenyeji katika taifa hili wamepatikana katika hali ya kutojiandaa kupokeza uongozi. Hii ndio maana wanashangaa na kuhisi kuwa si wakati mwafaka wa kupokeza uongozi wa taifa.

Kwa upande mwingine, mfichamo unaojitokeza katika kauli hii ni kuwa viongozi hawa wenyeji wana bidii ya kuendelea kubaki uongozini. Hili litaezekana iwapo Sizonje atakubali kula chakula anachokipikiwa ili alale. Hawa ni viongozi wanaoishi kubaki madarakani kwa rushwa wanazozitoa kwa wanaojaribu kuwapinga. Hii ndio maana wanaomba kujua iwapo anatumia vyakula *vya nazi* au *vya mafuta.*

Mifichamo katika kauli hii inaashiria wazi namna viongozi wa mataifa ya Afrika wanavyopinga mabadiliko katika jamii zao. Viongozi wapya, mitazamo mipya ya kufanya mambo au namna mpya za kimaendeleo zinapingwa na kukataliwa kwa vyovyote vile hata ikiwa ni kulisha rushwa waasisi wa mitazamo hiyo mipya mradi wananyamazishwe.

(42) **Kuna sauti inajirudia mara kwa mara**

**Na hapa mlangoni kulikuwa na picha mbili kubwa**

**Moja picha, nyingine mchoro wa picha wa kwanza**

Sitiari ya sauti inayojirudia mara kwa mara na picha iliyoko mlangoni ni kauli zinazopinga kanuni ya ukweli katika utaratibu wa kimazungumzo. Msikilizaji analazimika kufikiria kuhusu maana za kimfichamo zilizoko katika ujirudiaji wa sauti hiyo pamoja na mtazamo wake kuhusu picha iliyoko. Ukweli wa kuchukulia kauli kuwa sauti inaweza kujirudia rudia bila ya sababu yoyote unatiliwa shaka, pamoja na ile taswira ya picha ya mlangoni ni shaka nyingine. Hii ndio maana mfichamo wa kauli hii ni faradhi kwa msikilizaji.

Mfichamo unaojitokeza katika kauli hii ni kuwa, sifa za viongozi katika taifa hili zimekuwa zikijirudia mara kwa mara. Hii ina maana kuwa wananchi hawana matumaini yoyote kuhusu walioko madarakani kushughulikia shida zao, kwa sababu wana sifa zinazofanana na watangulizi wao ambazo hazikupendeza.

Ile taswira ya picha iliyoko mlangoni isitoshe inasisitiza kuwa sifa za viongozi walioko mamlakani zinaelekea kufanana na sifa za waliotoka madarakani, sifa za unyanyasaji na ubinafsi. Sizonje ni mgeni na hana sifa hizo hivyo basi wenyeji wanamshangaa kwa kuwa wamezoea viongozi wanaopokezwa uongozi kufanana na watangulizi wao.

## 4.4 UPINGAJI WA KANUNI YA IDADI

(43) **Tulikaa barazani, tukasikia kelele**

**Kelele toka ndani, mtu anaruka dirishani**

Kauli hii inapinga kanuni ya idadi ambayo inamhitaji mzungumzaji kutoa habari zote muhimu ambazo zinahitajika na msikilizaji ili kuelewa kauli fulani. Kimsingi, kauli isiwe na utata wa kueleweka. Katika kauli hii, msimulizi anakosa kutoa habari zaidi kuhusu kelele alichokisikia na kilichotokea ndani ya nyumba hii ambacho kinamfanya mhusika aruke kutoka ndani kupitia dirishani.

Msanii hapa anatumia mbinu ya taswira kumjengea msikilizaji picha akilini ya namna mambo yanavyofanyika katika nchi hii,kwamba, wananchi wameketishwa nche ya shughuli za nchi yao,

hawahusishwi katika mambo muhimu ya kujadili hatima yao. Ndani walipokaa wachache viongozi kumejaa vurugu na uhasama ambao umesitisha shughuli muhimu za kushughulikia matarajio ya wananchi, ndio maana kuna kelele hadi watu wengine kutokea dirishani maana hawataki kutokea mlangoni waaonekane na wananchi waliowachagua.

Mfichamo huu unajenga maudhui ya uongozi mbaya kwa namna viongozi walivyowatenga raia wengine katika uundaji na utekelezaji wa sera muhimu za nchi yao. Katika muktadha mataifa ya Afrika mashariki, inadhihirisha namna wananchi walivyopuuzwa na viongozi wachache wabinafsi.

**(44) Sizonje chumba hiki naomba usiingie**

**Ukimaliza nitakwambia kwa nini**

Kauli hii inapinga kanuni ya idadi katika utaratibu wa mawasiliano. Msemaji anafaa kusema kauli ambayo inatoa habari muhimu, yaani asiseme mengi au kusema mambo ambayo hayatoi habari zote muhimu. Kauli hii haitoi habari zote muhimu na hivyo msikilizaji katika mazungumzo haya atalazimika kujenga mfichamo kutokana na kauli hii. Msimulizi hatoi sababu za kumzuia Sizonje kuingia chumba anachomwonyesha.

Mfichamo uliopo hapa ni kuwa, viongozi walio madarakani wanaz sekta ambazo hawangependa ziguswe au kutawaliwa na wageni. Huenda zikafichua uozo wao iwapo zitatawaliwa na watu tofauti. Maudhui ya matumizi mabaya ya mamlaka yanadhihirika katika mfichamo wa kauli hii.

**(45) Kuna sauti inajirudia mara kwa mara**

**Na hapa mlangoni kulikuwa na picha mbili kubwa**

**Moja picha, nyingine mchoro wa picha wa kwanza**

Msimulizi anatoa sitiari mbili ambazo zinarejelea jambo moja katika kauli moja. Hapa msimulizi anapinga kanuni ya idadi kwa haja ya kusisitiza hali halisi ya mambo katika taifa hili. Ujirudiaji wa sauti na kule kuwepo na picha mbili mlangoni zinazofanana ni ishara mbili zinazoleta dhana moja ya marudio. Mtindo huu wa kutumia lugha ndio unaopinga kanuni ya idadi ya kimawasiliano. Mathalan, msimulizi amesema zaidi ya anavyotakiwa kusema ambacho ni kinyume na kanuni ya idadi. Mfichamo hapa ni kwamba, msimulizi anataka kusisitiza swala kuwa viongozi wa taifa hili wana sifa zinazofanana na watangulizi wao na hivyo mkombozi wa raia wanyonge bado

hajapatikana. Huenda Sizonje ambaye anaonekana mgeni na sura zilizotangulia akawa mkombozi wao.

## 4.5 UPINGAJI WA KANUNI YA NAMNA

Kanuni mojawapo wa utaratibu wa kimawasiliano ni ile inayomhitaji msemaji kusema mambo wazi bila kuleta utata katika uelewekaji wa kauli za msemaji. Kwa hivyo, uelewekaji hutegemea namna kauli inavyotolewa na msemaji.

(46) **Najua, wimbo mbaya haufai kubembelezea mtoto**

**Na kamwe mtoto hawezi kuungua kwa kiazi kilichokuwa kwenye kiganja cha mama yake mzazi**

Msimulizi katika kauli hii ametumia methali mbili kwa namna ya kufuatana. Msikilizaji ambaye yupo katika utaratibu wa ushirikiano na msimulizi wa shairi hili huenda akatatizika kuelewa lengo la mfululizo wa methali hizi mbili. Kufululiza methali katika usemi kunazua utata na hivyo kuzuia uelewekaji wa kauli. Mfichamo unaishia kuwa namna rahisi ya kujinusuru kutikana na upingaji huu wa kanuni ya namna.

Mfichamo unaotokana na kauli hii ni kuwa ahadi nzito za uongo wanazoziimba viongozi ambazo hawatekelezi haziwezi kuwanyamazisha wananchi wanyonge wanaolia kwa mateso ya kila siku yanayotokana na uongozi mbaya wa viongozi hao.

(47) **Si unajua, harufu ya uzazi haiishi mpaka mtoto akue?**

Kanuni ya namna ya utaratibu wa kimasiliano inapingwa katika kauli hii kwa namna swali hili lilivyoulizwa. Hili ni swali la balagha ambalo linasababisha utata wa msikilizaji kuelewa anachokimaanisha msemaji.

Mfichamo unaojitokeza hapa no ni kuwa, kiongozi huyu mgeni anafafanuliwa majukumu yake ya kulea taifa na ahakikishe kuwa taifa limekuwa na kwamba majukumu ya ulezi hayatamwondoka hadi taifa hilo litakapopata kukua. Maudhui ya uwajibikaji yanajengeka kutokana na mfichamo huu.

## 4.6 UPINGAJI WA KANUNI YA UHUSIANO

Kimsingi katika kanuni ya uhusiano, msemaji anahitajika kutoa mchango wake kuhusiana na muktadha wa mazungumzo. Chochote kinachosemwa nje ya mazingira ya mazungumzo huwa kinapinga kanuni hii ya uhusiano.

(48) **Sizonje, ukiona tembo anaringa**

**Ujue mvua zinakaribia**

Mchango wa msimulizi wa shairi hili kutokana na kauli hii unapinga kanuni ya uhusiano. Kunakosekana uhusiano wa tembo anayeringa na mjo wa mvua pamoja na muktadha wa shairi hili la mjo wa mgeni na mazingira ya nyumba.

Mfichamo unaotokana na kauili hii ni kuwa kunao matumaini kutokana na mjo wa Sizonje kulikomboa taifa ambalo limekuwa na matatizo mengi ya uongozi. Maudhui ya matumaini yanajengeka kutokana na mfichamo huu.

(49) **Si unajua, harufu ya uzazi haiishi mpaka mtoto akue?**

Mchango huu wa msimulizi kupitia kauli hii unapinga kanuni ya uhusiano kwa kuwa, harufu ya mzazi na ukuaji wa mtoto haina uhusiano ya swala la nyumba na Sizonje. Kwa hivyo, msikilizaji analazimika kujenga mfichamo wa kauli hii.

Mfichamo unaotokana na kauli hii ni kuwa, mgeni Sizonje anajulishwa kuwa, majukumu ya kulea hayatamwisha hadi ahakikishe kuwa wananchi na taifa kwa jumla limepata kukua na kufikia kiwango cha kujitegemea lenyewe. Bila ya kufanya hivyo, taifa hilo litabaki na harufu ya uzazi milele.

## 4.7 HITIMISHO

Katika sura hii tumejadili namna matumizi ya mbinu mbali mbali za lugha yanavyopelekea kupinga kanuni ya ukweli, udadi, namna na uhusiano katika mzumngumzo. Vile vile tumechunguza mfichamo unaojengeka kutokana na kila mojawapo wa kauli zilizopinga kanuni za utaratibu wa kimazungumzo kisha tukaangalia namna mfichamo huo unavyochangia katika kuimarisha maudhui ya uzalendo, uongozi mbaya, uwajibikaji, ufisadi pamoja na mengine katika shairi hili.

## SURA YA TANO

## 5.0 MATOKEO YA UTAFITI, MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO

### 5.1 UTANGULIZI

Katika sura hii tutatoa maelezo kuhusu matokeo ya utafiti huu ambayo ni majibu ya maswali ya utafiti. Isitoshe tutatoa mahitimisho kisha tutoe mapendekezo yanayotokana na utafiti huu.

### 5.2 MUHTASARI WA MATOKEO YA UTAFITI NA HITIMISHO

Mtazamo wa kipragmatiki mitindo ni mtazamo unaopania kuunganisha taaluma ya isimu na fasihi kwa namna ya kutumia nadharia ya kiisimu kuhakiki mtindo wa lugha katika kazi ya kifasihi. Utafiti huu ulijikita katika kanuni za utaratibu wa kimazungumzo ili kuchunguza matumizi ya mbinu mbali mbali za lugha zinazopelekea upingaji wa kanuni hizo.

Kwa kutumia mtazamo wa kipragmatiki mitindo, utafiti huu ulichunguza mifichamo inayoibuka kutokana na kauli mbali mbali zinazopinga kanuni za utaratibu wa kimazungumzo. Isitoshe tulihakiki namna mfichamo unaoibuka kutokana na upingaji wa kanuni hizo unavyochangia katika kujenga maudhui mbali mbali katika mashairi ya *Nikipata Nauli* na *Sizonje.*

Utafiti huu ulipata kuwepo kwa upingaji wa kanuni za ukweli, idadi, namna na uhusiano katika kauli mbali mbali zinazotumika katika mashairi ya *Nikipata Nauli* na *Sizonje.* Matumizi ya kinaya na sitiari yalisheheni sana katika kauli za mashairi haya mawili. Kwa kutumia mbinu hizi mbili msanii alifaulu kufumba ujumbe na kumpa msikilizaji nafasi ya kuipa kauli maana mbali mbali.

Matumizi ya mbinu hizi mbili aidha yalisababisha kuvunjwa kwa kanuni ya ukweli katika utaratibu wa ushirikiano wa kimazungumzo na hivyo kuzua mfichamo wa kauli mbali mbali. Mbali na sitiari na kinaya, msanii ametumia chuku,

uradidi,methali, ucheshi pamoja na jazanda ambazo ni mbinu zilizofanikisha uvunjaji wa kanuni za uratatibu wa ushirikiano katika mashairi haya mawili.

Swala la muktadha katika utafiti huu lilikuwa la muhimu sana kwa kuwa lilitusaidia kutambua miktadha ya kauli mbali mbali na pale msanii alipotoa kauli ambayo haiendani na muktadha wa mazungumzo hayo, tuliorodhesha kauli hiyo kuwa imevunja kanuni ya uhusiano.

Kutokana na uchunguzi wetu, kulikuwa na uvunjaji mwingi wa kanuni ukweli katika mashairi haya mawili ikilinganishwa na kanuni nyingine za utaratibu wa ushirikiano wa kimazungumzo. Hii ilisababishwa na matumizi mengi a kinaya, jazanda, sitiari na lugha ya ishara.

Kutokana na mfichamo wa kauli katika mashairi yaliyotafitiwa, maudhui ya uzalendo, ufisadi, matumizi mabaya ya uongozi, unyanayasaji, tamaa na ubinafsi, matumizi mabaya ya mali ya umma, mapuuza ya viongozi, udanganyifu na ukatili yalijengeka. Hii inaonyesha kuwa, swala la umaaniho ni muhimu katika kujenga maudhui katika kazi za kifasihi.

Kwa kuhitimisha basi, tunaweza kudai kuwa, kutokana na mfichamo tumeweza kupata maudhui mengi yanayopitishwa kutokana na kauli za msanii katika mashairi haya mawili. Mfichamo kutokana na kauli zilizovunja kanuni za utaratibu wa ushirikiano ulichangia katika kutupea maana anuwai za kauli ambazo ni ujumbe kama unavyopokelewa na msikilizaji wa mashairi haya. Kwa hivyo dhana ya uvunjaji kanuni za utaratibu wa kanuni za ushirikiano wa kimazungumzo, muktadha asili na muktadha pokezi pamoja na matumizi ya lugha ya ishara ni mambo yanayotegemeana katika kuibuka na kujenga mfichamo wa kauli.

## 5.3 MAPENDEKEZO

Kutokana na upeo wa utafiti huu, hatukuangalia mchango wa maana ya viziada lugha vinavyotumiwa katika video za nyimbo za *Sizonje* na *Nikipata Nauli.* Tungependekeza watafiti wa baadaye washugulikie maana zinazoibuka kutokana na lugha za ishara na viziada lugha vya msanii pamoja na matumizi ya kiimbo katika nyimbo hizi.

Aidha katika utafiti wetu hatukuchunguza nyimbo zingine zamsanii huyu, tungependekeza watafiti wa baadaye kuchunguza uvunjaji kanuni na mfichamo katika nyimbo zingine za Mrisho.

Isitoshe swala la matumizi ya lugha katika nyimbo za Mrisho linaweza kuangaziwa kwa kutumia mitazamo ya kinadharia mingineyo.

KIAMBATISHO I: **Nikipata Nauli – Mrisho Mpoto**

**Kibwagizo**

Eeh mjomba eeh, x2

Bora kujenga daraja, kuliko ukuta

Chemchemi sitemi, ukitaka maji sharti uiname

Bora kujenga daraja, kuliko ukuta

Nikipata nauli, mjini nitakufuata

Eeh mjomba eeh x2

**Mazungumzo**

Pole sana mjomba, una kibarua kizito kutaka dunia kuwa kijiji, Hongera!

Kile kiitikio cha *globalisation* kimeimbwa vizuri sana japo hakijakaririwa,

Nasikia wageni wamefurahi sana kusikia sauti yako,

Tena wanafurahishwa na ule ubeti wa mwisho uliouongeza

Wa mbio zetu kutoka uhuru mpaka hapa tulipo

Mjomba hapa nyumbani tuna hadithi na misemo mingi kujihakiki,

Maana lake mtu halimtapishi

Lakini kufumbatia maji kama jiwe ni ujinga

Juzi walisema kwa kuwa ni wageni kitalani, tuwape muda,

Jana Tumbokali kashikwa na kuku wa jirani, mkasema imewauma sana, ila bado tuwape mu

Eti kidhibiti cha mwizi wa kuku sharti ashikwe na mjuzi au kipande cha mnofu

Eeh mjomba eeh x2

Mjomba, sina nia ya mbaya, lakini je, unaijua timu yako?

Maana tabia ni kama ngozi, hauwezi kuibadili

Na mtoto wa nyoka hafundishwi kuuma

Ukicheka na nyani utavuna mabua mjomba!

Masikini, mtu kwao, ugeni si kitu chema

Msimu wowote kuanza upya si ubaya,

Mbwa hafi akiona uvuko,

**Kibwagizo**

Eeh mjomba eeh x2

**Mazungumzo**

Eti wanaomba samahani,

Watarudisha uhai wa waliopotea kwa uzembe wao?

Watawanyanganya waliowapa masikio yetu kama zawadi?

Mjomba, *life is not a reharsal, it is a perfomance!*

Mchelea haki hatendi kweli, mjomba!

Tazama maisha yetu, utadhani mchezo wa kuigiza!

Migodi sita! Yote kwangu

Hekali mia moja! Najiandaa kustaafu nipate sehemu ya kupumzika

Mazihala je? Aah, aliyemwoa mtoto wa mjomba wangu, kakake na mamangu nikampa zawadi

Inauma sana!

Inauma sana kugawa malalio yetu kama zawadi, mjomba.

**Kibwagizo**

Bora kujenga daraja, kuliko ukuta

Chemchemi sitemi, ukitaka maji sharti uiname x2

Bora kujenga daraja, kuliko ukuta

Nikipata nauli, mjini nitakufuata x2

Mjomba,tazama kule!

Ile ni shule, na yule anayegawa visheti pale ni mwalimu!

Wengine watauza kesho, wamepeana zamu ya kuyanusuru maisha yao

Japo haipo kwenye mtaala wa shule, tukiona inasaidia tuipitishe tu.

Wala siwachongei, mkiwafukuza, wafukuze wote, majengo tufugie kuku

Labda ndilo tunaloliweza

Eti mchezea zuri, baya umfika, nani kasema?

Wangefanya nini ikiwa hawajui kesho yao?

Nachoamini mjomba, mgomba haushindwi na mkungu,

Kwani mkamatwa na ngozi si ndiye mwizi wa ng'ombe?

Vipi mpaka leo wapo?

Tena mabingwa wa nahau na methali kule kitalani, wana misamiati mipya siku hizi

" ukunikanyaga tu!" eeh

Hofu yangu, siwaoni kwenye nyama siku hizi,

Hata lile la kulala limepungua

Mawili,

Wanasoma sana miswada au kwa kuwa *live* runingani wanauza sura

*Anyway* tuyaache hayo, turudi kwenye mada yetu mjomba

Huku kwetu mjomba hali si shwari, kila kukicha, afadhali ya jana!

Watu hawajakuelewa

Nikipata nauli nitakuja kukunongoneza mjomba,

*Please*, tafadhali! Wacha maagizo mlangoni, maana siku hizi wanataka sifa kweli, hawachagui pa kupiga,

Utasikia,

Lilikuwa likipambana na polisi tukalishinda

Wapi?

Kumbe mpwao hana mipango ya kuinusuru nchi, mpaka zikufikia wewe, huku tia maji tia maji,

Tahamaki, uchaguzi huo, n'natania tu mjomba....

ila kweli nikipata nauli nitakuja,

**Kibwagizo**

eeh mjomba eeh x2

Bora kujenga daraja, kuliko ukuta

Chemchemi sitemi, ukitaka maji sharti uiname x2

Bora kujenga daraja, kuliko ukuta

Nikipata nauli, mjini nitakufuata x2

## KIAMBATISHO II: **Sizonje - Mrisho Mpoto**

**Kibwagizo**

Sizonje hii ndio nyumba yetu

Milango ipo wanapita madirishani

Sizonje ndio nyumba yetu

Milango ipo wanapita madirishani

Ingia uyaone, maajabu ya nyumba yetu x2

Tulikaa barazani, tukasikia kelele

Kelele toka ndani, mtu anaruka dirishani

Sizonje, karibu nyumbani kwetu

Uone maajabu ya nyumba yetu

**Mazungumzo**

Karibu sana Sizonje, hii ndo nyumba yetu

Tulipoficha mundu za kupondea wezi

Kwani, makaburi yaliofukuliwa lazima yazikwe upya?

Nyumba hii Sizonje ina vyumba vinne

Vitatu havifunguki, kimoja hakina mlango

Ijapokuwa kina watu ndani, na hawaongei kiswahili

Wenyeji wanalala sebuleni na walishazoea

Sizonje kule tulipotoka panaitwa jikoni

Huna haja ya kwenda kule, kumejaa mafundi wa kupika

Sasa hivi wanakupikia wewe ili ule ulale

Ukiamka muongee nini hasa ujio na dhima ya safari yako

Wanashangaa mbona ghafla

Samahani sana mgeni

Wapishi wameniomba kwamba

Nikuulize tena kwa kukuomba kwamba

Eti unapenda vya mafuta au vya nazi?

Wanataka kukuonyesha madoido katika mapishi yao Sizonje

Sizonje chumba hiki naomba usiingie

Ukimaliza nitakwambia kwa nini

Kuna sauti inajirudia mara kwa mara

Na hapa mlangoni kulikuwa na picha mbili kubwa

Moja picha, nyingine mchoro wa picha wa kwanza

Ninachokumbuka iliwahi kuandikwa

"USIYEMTAKA KAJA"

Hatukuwahi kuelewa maana yake

Labda kwa sababu ya ujio wako unaweza kutusaidia

**Kibwagizo**

Sizonje hii ndio nyumba yetu

Milango ipo wanapita madirishani

Sizonje hii ndio nyumba yetu

Milango ipo wanapita madirishani

Ingia uyaone, maajabu ya nyumba yetu x2

**Mazungumzo**

Najua, wimbo mbaya haufai kubembelezea mtoto

Na kamwe mtoto hawezi kuungua kwa kiazi kilichokuwa kwenye kiganja cha mama yake mzazi

Njoo huku uone Sizonje

Si unajua, harufu ya uzazi haiishi mpaka mtoto akue?

Sawa, Sizonje, huu hapa ni ua

Lile pale ni shimo la taka

Na kile pale ni choo

Kinachotutisha na kutuogopesha zaidi

Wanaoishi humu ndani hawajawahi kutupa taka

Wala kwenda chooni

Kama ukiwa makini

Kwa nje utasikia sauti za makundi ya watu

Wengi ni vijana, wana bahasha za khaki mikononi

"KAMA HAMTUPI TAKA SHIMO HILI MLICHIMBA LA NINI?"

Lakini pia kwenye sauti zao, Sizonje

Kuna watoto, wazee na kina mama

Ukiunganisha sauti zao ndio unapata hizo kelele

Ninavyosikia, ila sina uhakika

Waliambiwa kihistoria nyumba hii ni ya kwao

Na wana haki ya kutupa taka na kutumia choo hiki

Sasa, njoo nikuonyeshe huku uchochoroni

Uone maajabu mengine ya nyumba hii

Sizonje, ukiona tembo anaringa

Ujue mvua zinakaribia

Kibwagizo

Sizonje hii ndio nyumba yetu

Milango ipo wanapita madirishani

Sizonje ndio nyumba yetu

Milango ipo wanapita madirishani

Ingia uyaone, maajabu ya nyumba yetu x2

Chimerah,R ( 1998) Kiswahili: Past,Present and Future Horizons. Nairobi University Press Nairobi.

Grice,H.P ( 1975) Logic and Conversation. In Cole,P &Morgan,J (Eds) *Studies in Syntax and Semantics III: Speech Acts*. New York: Academic Press, pp.183-198.

Habwe, J. & Karanja, P. (2004). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili.* Phoenix Publishers Ltd. Nairobi.

Hofmann, (1993) Realms of Meaning. An Introduction to Semantics. Longman Publishing. New York.

Igwedibia, E.A(2016) Analyzing the Political Speeches of Obama on Race and Economic Renewal in America in the Light of Theory of Conversational Implicature, *Mediterrenean Journal of Social Sciences*, MCSER Publishing. Rome, Vol. 7 No 3 S1, May 2016

Leech, G. (1983). Principles of Pragmatics. London: Longman.

Levinson, S. (1983) Pragmatics. Cambridge University Press.

Marmaridou, S.A. (2000) Pragmatic Meaning and Cognition. John Benjamins. Amsterdam

Mey, L.J (2000) Pragmatics: An Introduction. Blackwell Publishers, Massachusetts.

Mnyammpala, M.M (1964). Fasili ya Mashairi. *Swahili Committee Journal 33, 2*

Mugenda,O.M & Mugenda, A.G. (2003) Research Methods. Quantitative and Qualitative Approaches. Nairobi . Acts Press.

Njogu, K & Chimera, R(1999) Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu. Jomo Kenyatta Foundation. Nairobi.

Qun Li (2015) The Application of Cooperative Principle in Oral English Learning, *International Journal on Studies in English Language and Literature (IJSELL) Volume 3, Issue 1, January 2015, PP 39-48*

Robyn, C. (2004). Review of Rens Bod, Jennifer Hay, and Stefanie Jannedy 'Probabilistic linguistics' *Journal of Linguistics, 40, pp 181186 doi:10.1017/S0022226703272364*

Sperber,D &Wilson,D. (1986). Relevance, Communication and Cognition. Oxford: Blackwell.

Sperber, D & Wilson,D. (2007-2008) Relevance: Communication and Cognition. Wiley: Blackwell.

TUKI, (2006). English-Swahili Dictionary, 3rd Edition. Dar-es-Salaam

Wamitila, K.W (2003). Kamusi ya Fasihi. Nairobi: Focus Books.

Wamitila,K.W(2008) Kanzi ya Fasihi: misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi. Vide Muwa Publishers. Nairobi.

Yuan Li(2017) An Analysis of the Conversational Implicatures in Bishop's Poetry, *International Journal of Languages, Literature and Linguistics, Vol. 3, No.1 March 2017*

https://www.youtube.com/watch?v=lR6F-MlAtpc&pbjreload=10